

**ATHARI ZA SHENG KATIKA MATOKEO YA MTHANI WA KISWAHILI  
KATIKA SHULE ZA MSINGI MTAA WA KANGEMI**

**NA**

**DORICE KACHPELA**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA  
SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**NOVEMBA 2014**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

---

**DORICE KACHIPELA**

(MTAHINIWA)

---

TAREHE

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii tulioteuliwa ni chuo kikuu cha Nairobi.

---

**DKT. AYUB MUKHWANA**

**DKT. JEFWA MWERI**

---

TAREHE

---

TAREHE

## **TABARUKU**

Kazi hii ninamtabarukia marehemu dadangu mpendwa Susan kwa juhudi zake kunilea na kunielimisha, kunihimiza haja na uvumilivu maishani, kunishauri na kuniunga mkono kwa lolote nililoazimia kulifanya.

Mungu aiweke roho yako mahali pema peponi.

## SHUKRANI

Namshukuru Mwenzi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kuitimiza ndoto yangu kupata shahada ya uzamili katika chuo hiki tajika cha Nairobi.

Shukrani zangu zisizo na kifani ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. A. Mukhwana na Dkt. J. Mweri kwa mawaidha, ushauri na mwongozo walionipa hadi nikakamisha kazi hii.

Shukrani pia nazitoa kwa wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili kupitia kwa nasaha zao. Miongoni mwao ni Prof. Habwe, Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Swale, Dkt. Mbatia, Prof. Kinene, Dkt. Mbuthia, Dkt. Zaja na Bw. Muungania.

Aidha, nawashukuru wenzangu ambao tulikuwa pamoja nao katika safari hii ya usomi wa shahada ya uzamili. Sikola, Magdaline, Jane, Ruth, Julius, Dancan, Tsuma, Vincent, Grace, Furaha, Mariam, St Teresia, Jael, Karanja na Nyangeri.

Heko na shukrani nawatunukia mume wangu Wycliffe na wanangu Denis, Morine, Alvin, Denzel na Angela. Ninashukrani isiyo na kifani haswa kwa Wycliffe alinihimiza kila mara maisha yaliponisonga sihaba.

Alistahimili upweke, ukiwa na kuyatekeleza majukumu ya baba na mama wakati wa masomo yangu. Mungu akutunuku maisha si haba.

Mwisho nawashukuru wazazi wangu marehemu baba Joseph na mama Paulina. Kwa mama Paulina mola akupe maisha marefu.

## YALIYOMO

|                |      |
|----------------|------|
| Ungamo.....    | ii   |
| Tabaruku ..... | iii  |
| Shukrani ..... | iv   |
| Yaliyomo.....  | v    |
| Ikisiri .....  | viii |

### SURA YA KWANZA:

|   |    |
|---|----|
| 1.0 UTANGULIZI .....                              | 1  |
| 1.1Tatizo la Utafiti .....                        | 1  |
| 1.2 Madhumuni ya Utafiti.....                     | 2  |
| 1.3 Nadharia Tete.....                            | 3  |
| 1.4 Sababu za Kuchagua Mada Hii.....              | 3  |
| 1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....                | 5  |
| 1.6 Msingi wa Nadharia.....                       | 6  |
| 1.6.1 Kipengele Cha Uainishaji.....               | 8  |
| 1.6.2 Kipengele cha Ujitambulishaji na Jamii..... | 8  |
| 1.6.3 Kipengele cha ujilinganishaji kijamii.....  | 9  |
| 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii .....           | 13 |
| 1.7.1 Lugha ya Sheng.....                         | 14 |
| 1.8 Njia za Utafiti.....                          | 19 |
| 1.8.1 Ukusanyaji data .....                       | 19 |
| 1.8.2 Uchanganuzi data .....                      | 20 |

### SURA YA PILI:

|  |    |
|--|----|
| 2.0 UUNDAJI WA LEKSIMU ZA SHENG .....                                    | 21 |
| 2.1 Ukopaji na Utohozi .....   | 22 |
| 2.1.1Ukopaji na Utohozi: Maneno ya Kiingereza.....                       | 24 |
| 2.1.2 Ukopaji na Utohozi: Maneno ya Kiswahili.....                       | 25 |
| 2.1.3 Ukopaji na Utohozi: Maneno ya Kikuyu. ....                         | 26 |
| 2.1.4 Ukopaji na Utohozi: Maneno ya Kifaransa, Kiluhya, na Kidholuo..... | 28 |

|  |    |
|--|----|
| 2.2 Mbinu ya Ukatizaji.....            | 30 |
| 2.3 Mbinu ya Uambishaji.....           | 32 |
| 2.4 Mbinu ya Ubadilishaji Silabi.....  | 34 |
| 2.5 Onomatopia: Tanakali za Sauti..... | 35 |
| 2.6 Upolisemia.....                    | 37 |
| 2.7 Ubunifu wa Leksimu.....            | 38 |
| 2.8 Akronimu.....                      | 40 |
| 2.9 Kaleki: Tafsiri Mkopo.....         | 41 |
| 2.10 Uhulutishaji.....                 | 42 |
| 2.11 Uambatishaji.....                 | 44 |
| 2.12 Unyumbuzi Kapa.....               | 45 |
| 2.13 Ujenzi Ghairi.....                | 46 |
| Hitimisho.....                         | 48 |

### **SURA YA TATU:**

|  |    |
|--|----|
| 3.0 NYENZO ZA UJIFUNZAJI WA SHENG..... | 49 |
| 3.1 Vyombo Vya Habari.....             | 50 |
| 3.1.1 Redio.....                       | 50 |
| 3.1.2 Televisheni.....                 | 53 |
| 3.2 Wazazi.....                        | 55 |
| 3.3 Walimu.....                        | 57 |
| 3.4 Ndugu.....                         | 60 |
| 3.5 Wanafunzi.....                     | 63 |

### **SURA YA NNE:**

|  |    |
|--|----|
| 4.0 UCHANGANUZI WA DATA ZA MATOKEO YA MITIHANI.....  | 65 |
| 4.1 Kielelezo Cha Kwanza Cha Insha: Sheng.....       | 65 |
| 4.1.1 Tafsiri Ya Kielelezo Cha Kwanza Cha Insha..... | 66 |
| 4.2 Kielelezo Cha Pili Cha Insha: Sheng.....         | 68 |
| 4.2.1 Tafsiri Ya Kielelezo Cha Insha Ya 2.....       | 69 |
| Hitimisho.....                                       | 76 |

**SURA YA TANO:**

|   |    |
|---|----|
| 5.1MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....       | 78 |
| 5.2 Mambo Ibuka.....                      | 83 |
| 5.3Mapendekezo Ya Utafiti.....            | 84 |
| MAREJELEO .....                           | 86 |
| KIAMBATANISHO I::KIAMBATISHO HOJAJI ..... | i  |

## **IKISIRI**

Utafiti huu ulihusu Athari za Sheng katika matokeo ya mtihani wa Kiswahili katika shule za msingi mtaa wa Kangemi. Kazi hii imegawanywa katika sura tano, Katika sura ya kwanza tumeangazia maswala muhimu ya utafiti wetu. Tumeelezea swala la utafiti, madhumuni na nadharia tete zilizotuongoza. Aidha, sababu za utafiti, zimeelezwa pamoja na upeo na mipaka. Mwisho, mbinu za utafiti zimebainishwa na uchanganuzi data kufanywa. Vile vile katika sura hii tumeweza kuangazia yaliyosemwa kuhusu Sheng na wataalam mbalimbali. Katika sura ya pili tumeangazia mbinu mbalimbali ambazo wanajamii wa lugha ya Sheng huzitumia katika kuunda misamiati yao.

Aidha katika sura ya tatu tumeshughulikia nyenzo mbalimbali ambazo wanafunzi wa shule za msingi hujifunza Sheng kutokana nazo. Sura ya nne nayo tumechanganua data za matokeo ya mtihani ya Kiswahili ya kitaifa. Utafiti wetu umeweza kuangalia matokeo ya shule nne katika mtaa wa Kangemi. Sura ya tano ambayo ni ya mwisho, tumejikita katika matokeo ya utafiti, mahitimisho, mambo ibuka pamoja na mapendekezo ya utafiti wa baadaye.



## **SURA YA KWANZA**

### **1.0 UTANGULIZI**

Sura hii inatoa habari za kimsingi kwa mambo mengi ambayo tunalenga katika utafiti huu. Baadhi ya mambo hayo ni pamoja na tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yalioandikwa kuhusa mada hii, msingi wa kinadharia na mbinu za utafiti. Utafiti huu utahusu lugha ya Sheng kama chanzo cha matokeo mabaya ya mtihani wa Kiswahili katika shule za msingi nchini na mtaani wa Kangemi. Sehemu za miji nchini Kenya zina watu wengi kutoka katika matabaka tofauti tofauti. Nairobi kama miji mingine ya Kenya ina watu wengi sana. Watu hawa hupatika katika mitaa duni na pia katika mitaa ya kifahari. Miongoni mwa mitaa hii duni ni pamoja na mtaa wa Kangemi. Sehemu hii ina vijana wengi wanaoipenda na kuienzi lugha hii ya Sheng. Miongoni mwa vijana hawa wamo pia wanafunzi wa shule za msingi. Matumizi ya Sheng kwa vijana hawa huenea hadi shuleni ambako lugha ya Kiswahili inafaa kutumika kama lugha ya mazungumzo na tena kama moja wapo ya lugha inayotahiniwa katika mtihani wa kitaifa wa KCPE. Hivyo, katika utafiti huu tunachunguza mchango au michango ya Sheng katika ufunzaji wa Kiswahili Kenya.

### **1.1 Tatizo la Utafiti**

Lugha ya Kiswahili ni lugha ambayo imepewa hadhi ya kuwa lugha ya taifa na vile vile kuwa lugha ya kiofisi. Hii ina maana kwamba lugha hii ina haki ya kutumika kama lugha ya kuwaelekeza wanafunzi shuleni, katika kutimiza shughuli zao za kila siku. Ikumbukwe kwamba, lugha hii vile vile hutahiniwa katika kila kiwango cha elimu hapa nchini Kenya. Hata hivyo ipo athari ambayo inaelekea kuyalemaza majukumu msingi ya lugha hii hasa pale shuleni. Athari hii

inatokana na lugha ya Sheng. Sheng ni kama kijilahaja cha Kiswahili, ila si Kiswahili sanifu. Kijilahaja hiki kina wafuasi wengi wakiwemo wanafunzi wa shule za msingi. Hivyo, athari ya kijilahaja hiki pia zimeanza kutumika shuleni kama lugha elekezi na baadhi ya walimu walio kati ya umri wa miaka 25-35. Leksimu zake zimeoanishwa pamoja na zile za Kiswahili sanifu hivi kwamba linakuwa ni jambo tata kwa wanafunzi kutofautisha kati ya leksimu za Kiswahili sanifu na zile zisizokuwa za Kiswahili sanifu. Kwa kawaida maswali ya Kiswahili sanifu ndiyo huletwa katika mitihani ya somo la Kiswahili, na hasa somo la uandishi wa insha. Hivyo basi iwapo wanafunzi wataishia kuchanganya leksimu za lugha mbili na zenye uamilifu tofauti katika uandikaji wa insha, basi matokeo yake yatakuwa hasi. Hapa ndipo tatizo letu la utafiti lilipo. Yaani tutajikita katika kutaka kubaini kama kweli matumizi ya Sheng huathiri matokeo ya somo la Kiswahili shuleni au la. Pia katika utafiti huu tutaongozwa na maswali yafuatayo:

1. Je, sheng hukuza msamiati wake kivipi na kama ukuzaji huu hufanikisha mawasiliano?
2. Je, ni mambo gani yanayojitokeza katika mazingira ya shule ambayo huwa kielelezo kwa wanafunzi katika kujifunza na kuitumia sheng?
3. Je, matumizi ya sheng yameathiri matokeo ya somo la kiwahili?

## **1.2 Madhumuni ya Utafiti**

Utafiti huu utaongozwa na madhumuni yafuatayo:-

- a. Kubaini kama Sheng hukuza msamiati wake ili kufanikisha mawasiliano mwafaka miongoni mwa wanajamii lugha husika jinsi ifanyikavyo katika lugha nyinginezo.
- b. Kubaini kama vipo vigezo katika mazingira ya mwanafunzi ambavyo huwa kielelezo chake cha kujifunza, kuzungumza na kuikuza lugha ya Sheng.

- c. Kutathmini kama matumizi ya Sheng yameathiri matokeo ya mitihani ya Kiswahili katika shule za msingi Kangemi.

### **1.3 Nadharia Tete**

- a) Sheng hukuza msamiati wake ili kufanikisha mawasiliano mwafaka miongoni mwa wanajamii lugha husika jinsi ifanyikavyo katika lugha nyinginezo.
- b) Vipo vigezo katika mazingira ya mwanafunzi ambavyohuwa kielelezo chake cha kujifunza, kuzungumza, na kuikuza lugha ya Sheng.
- c) Matumizi ya Sheng yameathiri matokeo ya mitihani ya Kiswahili katika shule za msingi Kangemi.

### **1.4 Sababu za Kuchagua Mada Hii**

Sababu zetu za kuufanya utafiti huu ziliongozwa na madai mengi ambayo yametolewa na wataalam, wanataaluma, wasomi na vyombo vya habari kuhusiana na Sheng. Matokeo mabaya katika mitihani ya kitaifa ya somo la Kiswahili yameweza kufungamanishwa na Sheng kwa muda mrefu sana. Kumekuwepo na tetesi hili haswa kupitia kwa vyombo vya habari kama vile radio, runinga na magazeti. Wapo pia wanataaluma ambao wamewahi kuandika makala mbalimbali yanayohusiana na lugha hii ya Sheng. Hata hivyo hatukupata kushuhudia mwanataaluma yeyote yule ambaye ameandika makala yanayoihusisha lugha ya Sheng na matokeo mabaya ya mitihani ya Kiswahili katika shule za msingi. Hii ndio sababu ambayo ilituongoza katika kulifanyia swala hili utafiti.

Kulingana na waziri wa elimu kutokana na standadimedi Waziri wa Elimu Kenya alidai kwamba Sheng imechangia pakubwa kuwepo kwa matokeo mabaya ya Kiswahili katika mitihani ya kitaifa ya shule za msingi. Madai kama haya yamekuwepo pindi tu matokeo ya mitihani ya K.C.P.E yatangazwapo.

Waziri huyu anadai kwamba matokeo haya yamesababishwa na matumizi ya Sheng na watu wakuu katika nchi. Anasema kwamba Sheng ni lugha inayotumika sana na vijana wengi. Anadai kwamba idadi kubwa ya vijana mijini na katika makazi ya vibanda wanatumia Sheng kama lugha inayowaunganisha. Lugha hii ni kitambulisho chao hivyo basi huchangia kuenea kwake kwa kasi na kisha kusababisha matumizi ya lugha hii shuleni. Hatima yake huwa ni matokeo mabaya ya Somo la Kiswahili. Waziri huyu anadai kwamba kuenea kwa Sheng ni tatizo ambalo linafaa kushughulikiwa kwa haraka kwani tusipofanya hivyo lugha ya Kiswahili na Kingereza zitaendelea kuathirika katika mitihani ya kitaifa. Madai haya tunakubaliana nayo haswa tunapolinganisha matokeo ya shule za mashambani na yale ya shule za mijini. Shule za mashambani hufanya vizuri katika mitihani yao ya somo la Kiswahili kuliko zile za mjini Nairobi. Kule mashambani lugha ya Sheng haijapenya sana jinsi ilivyo hapa mjini. Ni kwa sababu hii utafiti huu unafanywa ilikubaini haya.

Vile vile utafiti huu utaangazia baadhi ya mambo yalioangaziwa kuhusu lugha ya Sheng. La ziada ni kwamba utafiti huu unaenda kuwasaidia washika dau wote katika Nyanja ya elimu kujua kama kweli Sheng inachangia matokeo mabaya katika shule za msingi au la. Kulingana na waliyoyasema wanataaluma wengi, lugha hii ya Sheng ina athari zake katika jamii. Ambalo

halijazungumziwa na wataalamu huwa ni kama kweli athari hizi hujidhihirisha katika matokeo ya somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi.

### **1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti wetu umejikita katika mipaka ya isimujamii na jinsi ambavyo lugha hii ya Sheng imesababisha matokeo mabaya katika mitihani ya kitaifa nchini Kenya. Tuliamua kutathmini Sheng kwa sababu lugha hii ni lugha inayotumiwa na vijana wengi wanaopatikana katika kaunti nzima ya Nairobi. Pia twaweza kusema kuwa Nairobi ndio chanzo cha lugha hii, na vile vile ndiyo kaunti yenye wanafunzi walioathirika zaidi kulingana na utafiti wetu. Lugha hii ya Sheng inazidi kukua kila uchao kwa sababu idadi ya vijana nayo inazidi kuongezeka.

Kimsingi, ni kuanzia darasa la sita, saba na nane ambapo vijana wengi nchini Kenya huanza kutayarishwa kwa ajili ya mtihani wao wa kitaifa wa darasa la nane. Vile vile ni wanafunzi wenye umri wa madarasa haya ambao huwa na mazoea yaliyokita ya matumizi ya Sheng katika mawasiliano yao ya kila siku. Hivyo, utafiti wetu unalenga katika kaunti ya Nairobi kwa sababu kaunti hii ya Nairobi ndiyo makao makuu ya Kenya. Hivyo basi mambo yote yanayokihusu Kiswahili katika kaunti zote za Kenya huweza kuwasilishwa katika kaunti hii ili yatafutiwe suluhisho mwafaka. Miongoni mwa mambo haya ni matokeo mabaya ya mitihani ya somo la Kiswahili katika shule za msingi. Hivyo, utafiti wetu unaenda kukita tu, katika kutathmini kama kweli lugha ya Sheng inachangia kuwepo kwa matokeo mabaya ya mitihani ya somo la Kiswahili katika shule za msingi.

Lugha ya Sheng ina chanzo chake mjini Nairobi. (Abdulaziz na Osinde (1947), Mukhwana (2008), (2014), Mzungu na Mbaabu (2006). Ni kutokana na madai ya wanataaluma hawa ambapo tumeamua kuufanya utafiti huu mjini Nairobi na, katika mtaa wa Kangemi. Katika utafiti huu hatujajishughulisha na madarasa mengine ila tu, darasa la nane. Sababu yetu ya kufanya hivi ni kuwa, matokeo ya Kiswahili ya darasa la nane ndiyo huangaziwa pakubwa ikilinganishwa na yale madarasa hayo mengine. Vile vile, wanafunzi wa darasa la nane ndio huonyesha kuathiriwa pakubwa na matumizi ya Sheng ikilinganishwa na wote wa madarasa mengine ya shule za msingi.

Ingawa yapo madai kwamba Sheng pia imeathiri matokeo ya mitihani kwa wanafunzi wa shule za upili lakini huko hatujaenda. Hii ni kwa sababu utafiti wetu haukiti mizizi yake katika shule za upili ila katika shule za msingi.

## **1.6 Msingi wa Nadharia.**

Utafiti wetu unajikita katika nadharia ya kitambulishi jamii. Nadharia hii iliasisiwa nao Henri Taifel na John Turner (1979). Wataalamu hawa walipendekeza kwamba kunayo michakato ya kiakili ambayo huhusika katika kuwatathmini watu wengine kama “sisi” au “wao.”

“Sisi” huwa katika kategoria ya kundi ndani na “wao” huwa katika kategoria ya kundi nje.

Kundi ndani ni kundi ambalo huwa tunajitambulisha kwalo na kundi nje ni kundi ambalo huwa hatujitambulishi kwalo. Mifano ya makundi katika jamii ambayo wanataaluma hawa waliyataja ni pamoja na;

## Mfano 1

- a) Rwanda : Wahutu na Watutsi
- b) Yugoslavia : Wabosnia na Wasarbi
- c) Ujerumani : Mayahudi na Wanazi
- d) Kandanda : Gor Mahiah na AFC Leopards
- e) Jinsia : Wanawake na Wanaume
- f) Matabaka : Tabaka la juu na la chini
- g) Ireland Kaskazini : Wakatoliki na Waprotestanti

Mifano hii inajumuisha mifano ya makundi nje na makundi ndani.

Katika mfano 1 mimi ni kundi ndani watu wengine ni kundi nje. Mashabiki wa A.F.C wanajichukulia kuwa kundi ndani ilhali wenzao wa Gor Mahia ni kundi nje. Vile vile kwa upande mwengine Gor Mahia wanajiona kuwa kundi ndani na wenziwe A.F.C kuwa kundi nje. Makundi haya mawili yanajaribu kubakia ndani hivyo basi kuzua ukinzani mkali. Katika Sheng vile vile kuna kundi ndani ambalo ni vijana wanaozungumza Sheng ilhali wenzao wachache wasiozungumza Sheng ni kundi nje. Katika mifano hii kila kundi katika jozi lake linajichukua kuwa kundi ndani na kundi kinzani kuwa kundi nje, kundi ndani hujiona kuwa bora zaidi kuliko kundi nje. Tathmini hii hutendeka katika mpangilio mahususi. Wataalam hawa walipendekeza vipengele vitatu ambavyo hutumika katika kutathmini makundi nje na makundi ndani katika jamii. Vipengele hivi ni kama vifuatavyo:

- a) Kipengele cha uainishaji.
- b) Kipengele cha kujitambulisha na jamii.
- c) Kipengele cha ujilinganishaji kijamii.

### **1.6.1 Kipengele Cha Uainishaji**

Katika kipengele hiki cha kwanza wataalam hawa wanasema mtu huainisha vitu katika mazingira yake ndiposa aweze kuvielewa na kuvitambua vyema. Mbinu hii huwa nzuri kwani hutusaidia katika kuwaainisha watu wa jamii zetu katika makundi mbalimbali. Katika uainishaji huu, nasi pia hujipata tumejiainisha kwa kujua au pasi kujua. Mara kwa mara huwa tunawaainisha watu kwa misingi ya kijamii ifuatayo: viongozi, weusi, weupe, Mkenya, mwalimu na mwanafunzi. Tunatumia viainishi hivi kwa sababu vina umuhimu katika jamii. Katika kuwaainisha watu katika kategoria tofauti, kipengele hiki hutuwezesha kuelewa yanayotuhusu kwa kufahamu kikundi tunachojitambulisha nacho. Kwa kawaida, binadamu hujitambulisha na kikundi katika jamii ambacho kulingana naye, huwa na hulka nzuri pamoja na mienendo bora inayolandana na hulka zake. Hata hivyo kuna watu wengi katika jamii ambao huweza kujiainisha katika makundi zaidi ya moja.

### **1.6.2 Kipengele cha Ujitambulishaji na Jamii**

Kipengele cha pili ni kipengele cha kujitambulisha na jamii. Wataaluma hawa wanasema kuwa, kwa kawaida huwa tunafaa kujitambulisha kwa kitambulisho cha kikundi ambacho tunajihusisha nacho na kuwa sehemu yetu. Kwa mfano ikiwa umejitambulisha kama Mkristo, utajaribu kuyatenda mambo au mienendo yako iwe ni kama ya Mkristo. Baada ya muda fulani utajikuta umebadilika na kutenda mambo yanayokubalika na kuhuzishwa na kaida za dini hiyo. Katika kutenda mambo haya utajihisi kwamba umebadilika, hali yako na pia hadhi yako katika jamii imepanda. Kila ulitendalo utalitenda kwa ustaarabu na motisha ya hali ya juu, hata kama unalolitenda si la haki mbele za umma, au makundi mengine katika jamii



### **1.6.3 Kipengele cha ujilinganishaji kijamii**

Hiki ndicho kipengele cha mwisho. Katika utaratibu ule wa kujianisha kama sehemu ya kikundi fulani na baadaye umejitambulisha na kikundi hicho kwa kufuata mienendo na kaida zake na kuonekana kama mmoja wa kikundi hicho kulingana na kaida zote au ukubaliano wa kikundi hicho, basi huna budi kujilinganisha na makundi haya mengine yaliyo katika jamii. Kwa kufanya hivyo, huwa tunawaona wanajamii wa makundi hayo mengine kama wasiofaa au wanaotenda mambo yaliyopitwa na wakati. Kwa kawaida kikundi chetu ndicho huwa bora na bora hata zaidi. Hali hii huishia kuzua makundi kinzani katika jamii. Kila kundi hujaribu kuwa kundi bora katika jamii kuyaliko hayo makundi mengine. Kila mwanajamii wa kundi fulani huchangia pakubwa katika mchakato huu. Kuwepo kwa makundi mawili kinzani katika jamii kuna madhara ya aina yake haswa wanapokutana pamoja Nadharia hii ya kitambulishi jamii inaingiliana sana na swala la utafiti wetu. Yaani ili kuwepo kwa ukinzani wa mambo au makundi mawili katika jamii, ni lazima kuwe na sababu msingi inayochangia ukinzani huo kuwepo. Ili tuelewe zaidi jambo hili hebu tutazame mfano ufuatao.

#### **Mfano 2**

##### **Kandanda: AFC na Gor Mahia**

Mfano huu unaonyesha kwamba kuna ukinzani kati ya timu hizi mbili za kandanda. Ukinzani kati ya timu hizi mbili unasababishwa na ligi ya Kenya. Ligi ya Kenya ndiyo inayosababisha makundi haya mawili au timu hizi mbili kuwa kinzani. Kama tujuavyo mshindi katika mashindano yoyote yale hutuzwa baada ya ushindi. Kutokana na ushindi huo, hadhi ya mashabiki na wachezaji wa timu husika huimarika. Kikundi husika hunufaika kifedha na pia kihadhi. Vile vile timu shindi huweza kupata fursa ya kushindana na timu zingine za nje au

kupata mapendeleo fulani kutoka kwa wenye kilabu au mashabiki. Wachezaji na mashabiki hufurahishwa sana pale timu yao hupata hadhi na pia kutambulika katika jamii. Kwa upande mwingine timu iliyoshindwa husononeka, na hufedheheka machoni pa watu. Wakati mwingine wao huenda wakapigwa na mashabiki kama sio kutusiwa. Mkufunzi wa timu iliyoshindwa huenda akapigwa kalamu ilhali wachezaji wa timu iliyoshinda huenda wakahifadhiwa. Hadhi yake hupanda na kuenziwa na wengi mno katika jamii.

Kipengee cha ujilinganishaji kinajitokeza wakati timu hizi mbili kinzani zinapojichukua kuwa kundi ndani ni bora zaidi kuliko kundi kinzani. Mashabiki wa timu hizi wanajilinganisha na timu yao na kujiona kuwa bora zaidi kuliko timu kinzani. Mpishano huu huendelea na harakati hiyo ya kujitahidi kubakia ndani. Katika Sheng vile vile wanafunzi wanaozungumza Sheng wanajainisha na wenzao wanaoongea Sheng. Wale waziojua au kuongea Sheng wanachukuliwa kuwa kundi nje. Tunapolinganisha mfano huu na hali ilivyo shuleni katika mtaa wa Kangemi watumizi wa sheng ambao ni wengi huchangia kuadhilika kwa matokeo ya mtihani wa Kiswahili. Hivyo, katika utafiti huu wetu tutathamini kama Sheng ni kisababishi cha kuwepo kwa ukinzani fulani kati ya lugha ya Kiswahili na Sheng hasa pale mwanafunzi anapojaribu kuzitumia lugha hizi mbili katika mitihani yake ya kitaifa.

Sheng kama lugha inayopendwa na vijana nchini Kenya imeathiri matokeo ya mtihani katika shule za msingi nchini. Hali hii inatokana na sababu kwamba wanafunzi wengi wameathirika pakubwa kwa kutumia lugha hii. Hivyo basi maandishi na mazungumzo ya wanafunzi hawa yameathirika pakubwa. Lugha ya Sheng imeomba istilahi nyingi za Kiswahili na kuziingiza katika matumizi yake. Hali hii mara nyingi huwakanganya wanafunzi hawa wasiweze kubaini

tofauti iliyopo kati ya leksimu za Sheng na zile zisizo za Sheng. Huu ndio ukinzani ambao hujikita katika akili za mwanafunzi wa shule ya msingi. Tazama mifano ifuatayo ya mazungumzo katika misingi ya Sheng:

### **Mfano 3**

Mifano

Sheng: Nibringie kitabu

Kiswahili: Nilettee kitabu

Sheng: Umenyita

Kiswahili: Umeelewa

Mfano wa kwanza, 'nibringie' ni neno 'bring' la kingereza. Ilhali nyita ni neno la Kikuyu linalomaanisha kuelewa. Katika Kiswahili lugha hii imesababisha maneno yasiyoeleweka na walimu au watahini na hivyo basi kuzusha utata mwingi katika nyanja ya elimu.

Maneno katika mfano wa tatu hapo juu yanatumika na vijana katika maongezi na maandishi ya shuleni hivyo basi kuzusha kutokuelewana kati ya walimu na wanafunzi wao wanaowataka kutumia Kiswahili sanifu kinachotahiniwa. Kwa upande mwingine, wanafunzi wanataka kujihusisha na walimu wanaoweza kuongea Sheng. Walimu kama hawa wapo ila ni wachache sana.

Mbali na walimu, wanafunzi wenyewe haswa wale wa mjini wanaoielewa lugha ya Sheng na wale wasioielewa Sheng huwa hawapatani kwa kawaida. Wale wasiojua Sheng huwa wanadunishwa kwa kutojua Sheng na hali hii huleta uhusiano mbaya. Hivyo basi tunaona kuwa Sheng kwa kiasi fulani imegawanya au kusababisha makundi mawili kinzani shuleni.

Walimu wanalalamika kuwa wanafunzi wengi ni weledi wa Sheng kuliko Kiswahili sanifu. Pia kuna tetesi kwamba lugha hii inasababisha kutokuwa kwa haraka kwa Kiswahili hasa nje ya mipaka ya Afrika Mashariki.

Nyumbani vile vile mambo ni yale yale ya ukinzani wa kimawasiliano. Kuna ukinzani kati ya wazazi na vijana. Mawasiliano yamekuwa tatizo kati ya wazazi na vijana walio katika shule za msingi ambao ni watumizi wa Sheng. Vijana wanatumia maneno yasioeleweka na wazazi wao nao hivyo basi wengine wanawachukulia kuwa wasimbeko. Vile vile mawasiliano haya huishia kuathiri masomo ya wanafunzi kwani ni vigumu kwa wazazi kuwasaidia katika kazi ya ziada nyumbani. Walimu wasioelewa Sheng hulazimika kuongea Sheng na hata wengi wao hutoa maelezo katika Sheng wakati wanapofundisha kwa minajili ya kuwafikia wale wasioelewa. Hivyo basi tunaona kuwa hii ni njia mojawapo ya kudunisha lugha ya Kiswahili.

Kwa sababu ya kuenea kwa Sheng kwa kasi, vyombo vya habari navyo havijaachwa nyuma katika ujainishaji huu. Vyombo hivi pia hutaka kujitambulisha na walio wengi. Kuna vipindi katika televisheni kama vile Tahidi high, Machachari katika Citizen Radio na pia Ghetto Radio. Vipindi hivi vinapendwa na wanafunzi wengi kwa sababu ya matumizi ya Sheng. Ukweli ni

kwamba vipindi hivi vinazidi kuongeza madhara katika lugha ya Kiswahili hivyo basi kuongezeka kwa matokeo duni katika mitihani ya kitaifa ya wanafunzi hao.

Shuleni wanafunzi wanaoongea Sheng na wanajitenga na wasioongea Sheng. Wale wanaoongea Sheng hujiona kuwa bora zaidi. Wanafunzi wanaoongea Sheng vile vile huwachukulia walimu wasioongea Sheng kama wasioelewa au kufahamu mambo ya usasa. Hivyo basi kuzua ukinzani kati ya walimu wanaowataka wanafunzi hawa kuongea lugha sanifu. Nyumbani mambo ni yale yale. Vijana hawa wanaoongea Sheng na kujihusisha na ndugu, marafiki na wazazi wenye umri wa miaka 25 hadi 35, wale wazazi wasiojua au kuzungumza Sheng wanadunishwa vile vile kuzua ukinzani kati ya makundi haya. Lamno ni kuwa kadri vijana hawa wanapoendelea kuongea Sheng ndivyo matokeo yao ya lugha ya Kiswahili yanavyoathirika.

### **1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii**

Kuna wataalamu wengi ambao wameandika kazi nyingi zinazohusu Sheng. Kazi za Wataalamu hao nyingi zimeegemea taaluma zao za kisosholojia, saikolojia, anthropolojia na hasa. Isimu kwa njia kubwa. Wengi walioandika juu ya mada ya Sheng wameongea juu ya Sheng kwa jumla. Hakuna aliyeangalia Sheng haswa katika matokeo ya mtihani wa shule za msingi. Hivyo basi tulionelea kuwa ni vyema tuandike juu ya Sheng na namna inavyoathiri matokeo ya Kiswahili katika shule za msingi na haswa katika kaunti ya Nairobi. Hata hivyo tuliangazia misimamo ya wanataaluma hawa inayohusiana na lugha hii ya Sheng.

### **1.7.1 Lugha ya Sheng**

Miongoni mwa wanataaluma ambao wamewahi kuandia makala yanayohusiana na Sheng ni pamoja na Iribemwangi na A. Mukhwana 2011. Iribemwangi na Mukwana, Katika kitabu chao cha Isimujamii, wanadai kuwa Sheng ni lugha ya vijana. Madai haya ya wanataaluma hawa wawili tuliweza kukubaliana nayo. Katika utafiti wetu, tulipata pia kubaini kwamba Sheng ni lugha ya vijana. Vijana hawa ni wale waliozaliwa mjini hasa walio kati ya umri wa miaka 10 hadi 35.

Iribemwangi na Mukhwana (2010) wanaitazama Sheng kama lugha ya msimu. Sharti tuelewe kwamba lugha ya msimu ina maaan kuwa ni lugha inayokuwepo kwa muda wa msimu fulani na kutoweka baada ya kipindi hicho kukamilika. Hata hivyo sikubaliani na wataalam hawa kwa kuichukulia lugha ya Sheng kuwa lugha ya msimu. Sababu ni kuwa lugha hii ya Sheng imekuwepo na inaendelea kukua kwa haraka mno. Kila inapokua ndipo inapozidi kupata umaarufu wake kutoka kwa vijana. Sheng ingekuwa lugha ya msimu ingekuwa imetoweka mnamo msimu huo uliotarajiwa au kuwepo. Vile vile lugha ya msimu ni ya kisaikolojia na ya kijamii. Asili ya lugha ya msimu inapatikana marekani miongoni mwa wamerika weusi na wamerika weupe. Maoni haya tunayapinga. Hatujawahi shuhudia kipindi bila Sheng. Kile tunaona ni kuongezeka kwa msamiati husika. Mabadiliko haya ya msamiati huwachanganya wanafunzi sana. Aidha madhara haya yanadhihirika wazi katika matokeo ya mtihani wa Kiswahili.

Madai ya wawili hawa tunakubaliana nayo. Vijana hawa ni wale walizaliwa mjini. Vijana hawa ni wengi mno katika mtaa wa kangemi. Wengi wao wanaongea Sheng inayoadhiri matokeo ya mtihani wa kitaifa.

Abdulaziz na Osinde (1996;44) nao wanadai kuwa Sheng ilianza katika mitaa ya Eastlands kati ya miaka ya 1960 na 1970. Lugha hii ilitumika na vijana katika vikundi vyao. Lugha hii ilitumika na vijana ili kujitenga na wakuu au wadogo zao wasijewakasikia na kuelewa mazungumuzo yao. Vijana hao waliishi pamoja na wazazi wao hivyo waliona ni bora wajiundie lugha ambayo wao wenyewe wangeielewa. Kadri miaka ilivyozidi kusonga ndivyo lugha hii ilivyozidi kukua na kuwa kama kitambulisho cha vijana hao na pia cha vikundi fulani vikubwa. Tunakubaliana na mawazo ya wawili hawa kwani ni vigumu kwa watu wazima na hasa walimu kuelewa Sheng. Vijana nao wanaiongea na kuienzi hivyo kuathiri masomo yao na matokeo ya mtihani katika mtihani wa kitaifa.

Mitchell na Antony (2005) katika kazi yao ya *Alectprime* nao wanadai kwamba Sheng ni istilahi mwiko hasa katika hotuba za kiserikali, kiofisi na zile za kawaida. Hotuba hizi hujumuisha watu wenye matabaka ya juu au wale walio na majukumu makubwa katika jamii. Lengo kuu la Sheng kupigwa marufuku katika hotuba hizi ni kuwa misamiati ya Sheng huchukua nafasi ya istilahi sanifu na zile muhimu zinazostahili kutumika katika muktadha maalum. Madai haya tunayaunga mkono pia. Sababu zetu za kuyaunga mkono zinatokana na ukweli kuwa, Sheng ni lugha mwiko katika ufunzaji na usomaji wa Kiswahili. Hivyo, iwapo mwanafunzi atatumia misamiati ya lugha hii katika mitihani yake ya Kiswahili basi hatafanya vizuri katika mitihani hiyo.

Juoni Philip Mahu (2009) naye anadai kwamba Sheng inatumiwa hasa na vijana na ni sehemu ya utamaduni pendwa nchini Kenya. Mwanatalumma huyu anadai kwamba lugha hii inakuwa kwa haraka mno. Anadai kwamba kukua huku kumesababishwa na madai kwamba maneno huingizwa na kuondolewa katika leksimu za Sheng kizazi baada ya kizazi, na majira baada ya

majira. Madai haya ya Mahu tulikubaliana nayo. Maana katika utafiti wetu tuliweza kubaini kwamba lugha ya Sheng ina visawe vingi mno. Visawe hivi hutokana na sababu kwamba maneno mengi huingizwa na kuondolewa katika matumizi ya lugha hii kulingana na mahitaji ibuka ya kizazi husika. Iwapo mambo haya yataendelea, msamiati huu utaingizwa katika Kiswahili hivyo basi kusababisha matokeo duni katika mtihani.

Githinji (2009), anadai kwamba Sheng imeenea na hata sasa inaongewa mashambani. Hata wanasiasa huiongea lugha ya Sheng katika mikutano yao ya siasa. Anaendelea kudai kuwa si kweli kwamba Sheng inaithiri matokeo ya masomo ya wanafunzi bali yote hayo yanasababishwa na idadi kubwa ya wanafunzi kutokana na kuanzishwa kwa elimu ya bure mwaka wa (2003). Madai ya Githinji tunayapinga kwani kabla ya masomo ya bure kuwepo Kiswahili kiliendelea kufanywa vibaya hasa mjini Nairobi. Isitoshe kuna shule za hapa mjini Nairobi zenye idadi ndongo ya wanafunzi na matokeo ya somo la Kiswahili ni yale yale mabaya. Vile vile kunazo shule za mashambani zenye idadi kubwa ya wanafunzi lakini matokeo yao ya somo la Kiswahili huwa mazuri sana.

Momanyi (2009) na Fishman (1996; 409) wanadai kuwa wanajamiilugha ya Sheng hutupilia mbali maadili, mienendo, ujuzi na tamaduni zao (hasa wale wa tabaka la kati) na kujiunga na vikundi mbalimbali katika jamii ambavyo hutenda mambo yavyo ya kisiri kwa kuitumia lugha hii kama chombo chao cha mawasiliano. Huko, wao wanapata kutambulika na kukubalika pasina jamii zao za awali. Kulingana na madai ya wanataaluma hawa tunakubaliana na wao kuwa hii ni lugha ya vijana. Ni lugha inayopendwa na vijana na baadhi ya vikundi walivyovizungumzia wanataaluma hawa hupatikana shuleni wanakosomea vijana wetu.



Asilimia kubwa ya vijana wa mjini Nairobi ni watumizi wa lugha ya Sheng. Sheng ndicho kitambulisho chao katika jamii na ndio utamaduni wao. Hivyo, ni vigumu sana kwao kuuachilia utamaduni na kitambulishi chao hata wanapokuwa shuleni. Utata huu hujidhihirisha pale wanapohitajika kutumia Kiswahili sanifu katika mitihani yao ya somo la Kiswahili. Tatizo hili husababishwa na kuathirika kwa vijana hawa katika maongezi, mandishi na matokeo ya lugha kwa jumla katika mitihani ya kitaifa.

Spypoulos (1987) anadai kwamba Sheng ilianza mnamo miaka ya hamsini na kutia fora katika miaka ya sabini. Spypoulos anasema hivyo kwa sababu ya kuyaona maandishi mengi katika makala, majarida na katika magazeti ambayo yalikuwa na habari zilizohusu Sheng. Habari za Sheng katika vyombo hivi vya habari zilianza kuonekana katika miaka ya sabini. Kulingana na utafiti wetu ni vigumu kubaini madai haya kwani hayana mashiko kuwa huu ndio ulikuwa mwanzo wa Sheng.

Mazrui (1995) Anasema kuwa Sheng ni wimbo wa vijana. Anaendelea kusema kuwa msimbo huu ulianza miongoni mwa vijana waliotoka katika jamii zenye mapato ya chini kiuchumi na waliishi katika mitaa duni ya mabanda iliyoko mashariki mwa jiji la Nairobi.

Anaendelea kusema kwamba vijana hawa waliishi katika chumba kimoja na wazazi wao. Hivyo basi walibuni msamiati wa siri ili wazazi wao ambao walilala nao chumba kimoja wasiyaelewe mazungumzo yao. Maoni ya mazrui yanalandana na ya wataalamu hawa wawili. Osinde (1986), Abdulaziz na Osinde (1997). Maoni haya tunakubaliana nayo. Vijana katika mtaa wa Kangemi

wana msamiati wao wanaotumia katika mazungumzo. Athari ni kwamba msamiati huu hutumika katika uandishi wa insha na hii huathiri matokeo ya mtihani.

Mitchell na Anthony (2005) katika makala ya *Aleet Prime* wanasema kuwa Sheng ni Istilahi mwiko katika hotuba za kawaida zinazojumuisha watu wa matabaka ya juu. Sababu ni kuwa leksimu za Sheng huchukua nafasi ya leksimu sanifu na muhimu sinazostahili kutumika katika miktadha maalum.

Kulingana na mwanataaluma Mazurui (1995) Anasema kuwa wamerika weusi ni watu waliopolekwa Marekani kuwa watumwa. Watu hawa waliishi katika hali hiyo ya utumwa mbaka wakati utumwa ulipopigwa marufuku. Huko marekani watu hawa walibaguliwa kwa misingi ya rangi. Wamarekani hawa weusi walinyanyaswa na kuteseka kiasi cha kunyimwa haki zao zote za kibinadamu. Kwa sababu ya mateso waliopitia iliwalazimu kuunda leksimu.

Leksimu hizi ziliakizi hali yao ya unyonge na unyanyasaji. Leksimu hizi walizitumia zikapata kuenea na mwishowe ziliweza kujulikana na wamarekani weupe waliotoka kwenye tabaka la juu na lenye uwezo wa kiuchumi.

Wamarekani weusi walipogundua kwamba jambo hili tayari wanalielewa wamarekani weupe, walibadilisha leksimu za awali na nyingine ampya ili wazidi kujitambulisha na kutengana na wamarekani weupe wenye uwezo wa kiuchumi. Hivyo basi tunaweza kusema au kuita lugha hii ya wamarekani weusi kama lugha musimu kwa sababu ilibadilika badilika kileksimu namna

mateso yao yalivyo zidi kuongezeka. Hii inaweza kuchukuliwa kuwa njia ya wamerikani weusi ambao hawakutaka kutangamana na weupe bali wabakie kwa kujitenga katika kundi lao.

Hivyo basi tunapolinganisha lugha hizi mbili yaana za Wamerikani weusi na Sheng hakuna uwiano wowote. Ukiwepo basi ni finyu mno.

Mazrui anadai kuwa Sheng ni lugha msimu ya vijana walioishi katika mitaa duni ya mabanda. Madai haya yanachukulia kwamba lugha ya Sheng ni ya vijana wanaotoka katika jamii maskini. Jambo hili nalipinga kwani Sheng inazungumzwa na vijana wote wanaotoka katika matabaka tofauti. Hivyo basi kwa sababu ya kukua na kuenea kwa lugha hii ya Sheng ni bora kama ingewekewa sheria za kisarufi kama ilivyo lugha nyingine. Lugha hii ya Sheng hukua na kubadilika kila uchao.

Kuna baadhi ya wataalam kama vile Filip Mahu (2009) wanaodai kuwa Sheng ni lugha inayozungumzwa na makundi mabaya kama vile wezi, wanyang'anyi, wabakaji, waraibu, walanguzi wa dawa za kulevya na kadhalika. Madai haya ni ya kweli na tunayaunga mkono.

## **1.8 Njia za Utafiti**

Katika utafiti huu tumetumia mbinu zifuatazo: kukusanya, kuhakiki na kutathimini data.

### **1.8.1 Ukusanyaji data**

Katika utafiti huu tulitumia mbinu ya ukusanyaji data. Kwanza tulisoma yaliyoandikwa kuhusu Sheng na vile vile athari zake katika jamii kama vile matokeo mabaya ya Kiswahili katika mitihani ya kitaifa. Pia, tuliweza kuwahoji wadau kuhusu kile wanachofikiria kuhusiana na athari

za Sheng kwa matokeo ya Kiswahili katika shule za msingi nchini Kenya. Ili kupata data ya kutosha kuhusiana na mada hii ya utafiti tulikuwa na hojaji. Hojaji hii tulitolewa kwa wadau wapatao mia moja. Hao wadau walichaguliwa kimakusudi katika kaunti ya Nairobi eneo la Kangemi. Hili lilifanywa kwa kuwa kihali halisi hatungeweza kutumia wadau wote katika utafiti wa sampuli hii. Hata hivyo waliotumika katika utafiti huu walikuwa wa jinsia zote mbili, wakitofautiana katika hali zao za kiuchumi na kijamii. Wote hawa walikuwa wanafunzi wa darasa la nane, walimu wao, wazazi na ndugu zao. Umri wao ulikuwa wa kati ya miaka 12 hadi miaka 35. Hii ilitokana na sababu kwamba vijana walio katika kategoria hii ya miaka ndio hujitambulisha kwa maongezi ya Sheng zaidi. Vile vile shule zilizotumika kupata data zilikuwa shule za msingi pekee. Hii ni kwa sababu utafiti wetu ulikita katika matokeo ya somo la Kiswahili katika shule za msingi tu.

Sababu nyinginezo ni kuwa, vijana hawa wa darasa la nane ndio wamo katika harakati ya kujua misamiati mipya katika lugha hii ya Sheng. Misamiati hii inapatikana kupitia njia tafauti tafauti kama vile vipindi vya redio na televisheni kwa mfano Machachari. Vipindi hivi huwalenga vijana. Hivi ni vipindi vinavyopendwa na vijana wa rika hili.

### **1.8.2 Uchanganuzi data**

Haya tuliyafanya baada ya kukusanya data. Tulichanganua data zetu kwa misingi ya nadharia ya kitambulishi jamii. Katika kuzichangamua, tulitumia mbinu ya ujiainishaji, ujitambulishaji na baadaye ujilinganishaji wa kijamii. Kupitia mbinu hizi tuliweza kufikia uwamuzi wa kukataa au kuzikubali haipotesia zetu. Yaani mbinu hizi zilitusaidia katika kuthibitisha mada yetu ya utafiti.

## SURA YA PILI

### 2.0 UUNDAJI WA LEKSIMU ZA SHENG

Habari za Sheng ni habari ambazo zimevitawala vinywa vya wataalamu, wasomi na wanataaluma wengi kwa muda mrefu. Wataalamu wote hawa wamekuwa wakizitoa habari ambazo zimekuwa zikihitilafiana kuihusu Sheng. Kati yao kuna wale walio na msimamo kwamba Sheng si lugha kwa sababu haina jamii wala mfumo wa kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na hata kisemantiki unaojibainisha kama ilivyo na lugha nyinginezo kama vile kiingereza. Kwa sababu ya ukosefu wa viwango hivi muhimu vya muundo wa lugha, basi inakuwa vigumu kwa wataalamu husika kuiainisha Sheng kama lugha na kuiwekea sheria za utenda kazi wake. Wale wanaoamini kwamba Sheng ni lugha wanafanya hivyo kwa madai kwamba Sheng inao uwezo wa kufanikisha mawasiliano miongoni mwa wanajamiilugha hii. Madai haya ndiyo tunayoyaunga mkono. Tunayaunga mkono kwa sababu lugha yoyote ile hufaulu kuitwa lugha iwapo ina uwezo wa kufanikisha mawasiliano miongoni mwa jamiilugha husika. Sheng inayo sifa hii ya msingi. Ufuatao ni mfano wa mawasiliano kati ya wanajamiilugha ya Sheng.

#### Mfano 4

Sheng: X. Magii joo! Wachanga za ovyo taim zingine.

Y. Ai buda! sijakuvako.

Tafsiri: X. Magdaline jamani! Mambo ya mzaha uwe ukiwachana nayo wakati mwingine.

Y. Bwana wee! Sijakudanganya.

Kutokana na mfano huu, ni wazi kwamba mawasiliano yaliweza kutimizwa kati ya mhusika X na Y. Yaani X na Y waliweza kuwasiliana katika mazungumzo yao. Hili linathibitishwa na ukweli kwamba X alimwuliza Y swali, naye Y akamjibu. Mawasiliano haya yalitendeka katika misingi ya lugha ya Sheng. Hivyo basi Sheng ina uwezo wa kufanikisha mawasiliano miongoni mwa wanajamiilugha waliohusika. Ni kwa misingi hii ambapo Sheng kama lugha huwa na uwezo wa kujitungia leksimu ili iweze kufanikisha mawasiliano baina ya wazungumzaji wake. Kati ya mbinu zote za uundaji wa maneno, lugha ya Sheng kimsingi hutawaliwa na mbinu mbili kuu za uundaji wa maneno. Utafiti huu umebaini kuwa, mbinu hizi ni ukopaji na utohozi, na ubunifu wa leksimu. Mbinu hizo zingine za uundaji wa maneno katika Sheng hasa hutegemia mbinu ya ukopaji na utohozi kama mhimili mkuu. Uundaji huu wa maneno haya ya Sheng waweza kuwa ndio huwa chanzo cha chimbuko la kutofanya vizuri kwa wanafunzi wa shule za msingi katika somo lao la Kiswahili. Ifuatayo ni mifano ya mbinu za uundaji wa maneno ambazo hutumiwa na wanajamiilugha ya Sheng.

## **2.1 Ukopaji na Utohozi**

Ukopaji ni hali inayojumuisha uhamishaji wa kipashio fulani kutoka lugha moja na kukiingiza katika lugha nyingine. Kwa hivyo, kuna lugha changizi na lugha pokezi. (Jefwa, 2010: 49).

Hock na Joseph (1996: 28), wanasema kuwa ukopaji ni uhamishaji wa leksimu mahususi au set ya leksimu au faridi fulani kutoka lugha moja au lahaja moja hadi nyingine. Kuna aina mbili ya ukopaji : ukopaji sisisi na ukopaji tohozi. Ukopaji sisisi ni pale ambapo leksimu fulani inahamishwa kutoka katika lugha changizi hadi lugha lengwa bila ya kufanyiwa marekebisho yoyote. Ukopaji tohozi nao hutokea pale ambapo neno lililokopwa hufanyiwa uhawilishaji ili lichukue muundo wa kimofolojia wa lugha kopa. Iribemwangi na Mukhwana (2011: 157) nao

wanafasiri maana ya neno utohozi kwa kusema kuwa utohozi hutokea pale ambapo leksimu imekopwa kisha ikafanyiwa marekebisho ya kifonolojia, kimofoloji au kisemantiki ili ifuate kanuni na muundo wa lugha kopaji. Kuhusu uhawilishaji, Matthews (1997:7) anasema kuwa uhawilishaji hutokea pale ambapo leksimu zinabadilishwa ili kuakisi mfumo wa kisauti wa lugha kopa.

Arlotto (1972:184) naye ana maoni kwamba baada ya ukopaji leksimu kopwa hupatiwa uasilia wa lugha kopa. Ni katika kupokea uasilia wa lugha kopa ndipo uhawilishaji hufanywa. Lugha kopeshi nayo huwa haipotezi neno hilo lililokopwa na lugha nyingine. Hartman na Stork (1972:29) nao wana maoni kwamba wakati mwingine leksimu iliyokopwa huhawilishwa. Ubayana wa maelezo ya wataalamu hawa ni kwamba uhawilishaji huwa sio jambo la lazima katika ukopaji wa leksimu.

Fronkin na Rodman (1988:309) pia wana maoni kuwa lugha zote ulimwenguni hukopa msamiati. Hivyo basi misamiati hujumuisha leksimu asilia na leksimu mkopo. Ukopaji ni mbinu ya uundaji wa maneno na ambao umetajirisha sana lugha za ulimwengu. Miongoni mwa lugha ambazo zimefaidika kutokana na mbinu hii ya uundaji wa maneno ni Kiswahili na Sheng. Kiswahili kina maneno mengi sana yaliyokopwa kutoka lugha kama vile Kiarabu, Kijerumani, Kiajemi na Kiingereza. Sheng pia imeziiga sifa hizi za Kiswahili kwa kukopa maneno kutoka kwa lugha kama vile Kiingereza, Kiswahili Kifaransa na lugha zingine za kienyeji kama vile Kikuyu, Kidholuo na Kiluhya. Ifuatayo ni mifano ya maneno ya Sheng yaliyokopwa kutoka katika lugha ya Kiingereza, Kifaransa, Kiswahili, pamoja na lugha zingine kama vile, Kidholuo, Kikuyu na Kiluhya.

### 2.1.1 Ukopaji na Utohozi: Maneno ya Kiingereza

Chimbuko la lugha ya Kiingereza ni nchi ya Uingereza. Wazungumzaji asili wa lugha hii huitwa Waingereza. Leo hii, lugha ya Kiingereza inazungumzwa katika mataifa mengi duniani kote. Lugha hii vile vile inatumika kama lugha ya mawasiliano karibu duniani kote, (Oxford Advanced Learners Dictionary 2010:486). Nchini Kenya lugha ya Kiingereza ilitangulizwa na wakoloni na wamishonari kabla ya vita vya kwanza na vya pili vya dunia. Jambo hasa lililochochea lugha hii kukita mizizi nchini Kenya ni kutokana na sababu kwamba, wamishonari waliitumia lugha hii sana katika shughuli zao za kuieneza injili na dini ya Kikristo.

Ifuatayo ni mifano ya leksimu za Kiingereza jinsi zilivyojidhihirisha katika jamiilugha ya Sheng, mtaani Kangemi.

#### Mfano 5

| <i>Leksimu mkopo</i> | <i>leksimi asili</i> | <i>maana</i> | <i>lugha changizi</i> |
|----------------------|----------------------|--------------|-----------------------|
| a) / Wode: /         | water                | maji         | Kiingereza            |
| b) / Ticha /         | teacher              | mwalimu      | Kiingereza            |
| c) / Mshi: /         | she                  | msichana     | Kiingereza            |
| d) / Keja /          | cage                 | nyumba       | Kiingereza            |
| e) / Ferare /        | fare                 | nauli        | Kiingereza            |
| / Tao /              | town                 | mjini        | Kiingereza            |
| f) / Cheki /         | check                | tazama       | Kiingereza            |
| g) / Mode: /         | mode                 | mwalimu      | Kiingereza            |
| h) / buku /          | book                 | kitabu       | Kiingereza            |



Ifahamike hapa kwamba, neno moja linaweza likakopwa na kuhawilishwa na zaidi ya lugha moja. Kwa mfano katika mifano hii ya maneno kopwa na toholewa kutoka katika lugha ya Kiingereza, lipo neno ambalo limekopwa na kutoholewa na zaidi ya lugha moja. Neno hili ni “buku.” Kimsingi, hili ni neno la Kiingereza “book,” lenye maana ya “kitabu.” Sheng imelikopa neno hili kwa mtindo wa ukopaji sisisi kutoka katika lugha ya Kiswahili, na kwa mtindo wa utohozi kutoka katika lugha ya Kiingereza.

### **2.1.2 Ukopaji na Utohozi: Maneno ya Kiswahili**

Nchini Kenya Kiswahili kimekuwa kikitumiwa kama lugha ya taifa kwa miaka mingi sasa. Lakini baada ya nchi hii kujipatia katiba mpya mnamo mwaka wa 2010, lugha hii ilipata hadhi mpya. Leo hii lugha hii sio lugha ya taifa tu, bali pia ni lugha rasmi. Hata hivyo utenda kazi wa hadhi hii mpya ya Kiswahili bado haujaanza kushuhudiwa vilivyo katika ngazi mbali mbali za serikali. Kinyume na hayo, Kiswahili ni lugha maarufu sana miongoni mwa Wakenya. Kinyume na kuwa lugha rasmi na lugha ya taifa, Kiswahili kimeanza kuwa lugha ya kwanza hasa kwa baadhi ya watoto wanaozaliwa mijini (kama vile Nairobi) na watoto wanaozaliwa katika familia za wazazi wenye asili ya makabila tofauti.

Hali hii ndiyo ambayo imechangia kuwapo kwa misamiati ya Kiswahili katika Sheng. Ifuatayo ni mifano ya leksimu za Kiswahili na jinsi ambavyo hujidhihirisha katika Sheng.

## Mfano 6

| <i>Leksimu mkopo</i> | <i>leksimu asili</i> | <i>maana</i>   | <i>lugha changizi</i> |
|----------------------|----------------------|----------------|-----------------------|
| a) Chapa             | chapa                | filisika/konda | Kiswahili             |
| b) Chuo              | chuo                 | shule          | Kiswahili             |
| c) Majuu             | juu                  | ulaya          | Kiswahili             |
| d) Katia             | kata                 | tongoza        | Kiswahili             |
| e) Mzae              | mzee                 | baba           | Kiswahili             |
| f) Mahewa            | hewa                 | muziki         | Kiswahili             |

Maneno haya ya Kiswahili hukopwa na lugha ya Sheng kisha hupewa maana mpya katika lugha hiyo. Kwa mfano, neno “chapa ni neno la Kiswahili lenye maana ya kutia adabu au kurudufisha. Lakini kando na maana yake ya msingi, neno hili limepata maana mpya katika lugha ya Sheng kama vile tumeonyesha katika jedwali hapo juu.

### 2.1.3 Ukopaji na Utohozi: Maneno ya Kikuyu.

Wakikuyu ni sehemu ya Wabantu na wanapatikana katika maeneo ya Afrika Mashariki, hasa nchini Kenya. Hili ndilo kabila kubwa zaidi ya yote nchini Kenya na lugha yao ya mama inajulikana kama Kikuyu (haya ni kwa mujibu wa mofolojia na fonolojia ya Kiwahili). Wao wenyewe hujiita “Agikuyu” na wanapatikana katika mkoa wa kati kwenye kitovu cha Mlima Kenya. Haya ndiyo maeneo yao ya asili tangu walipowasili nchini Kenya kutoka Afrika ya Magharibi. Inakisiwa kwamba idadi kamili ya Wakikuyu nchini Kenya ni watu 6,623,000. (I. Larsen 2009: wikipedia).

Leo hii Wakikuyu hawapatikani tu katika eneo la Mlima Kenya. Wao wamezagaa na kutawanyika katika kila pembe ya nchi ya Kenya. Vile vile, inaaminika kwamba asilimia kubwa ya wakaazi wa mji mkuu wa Kenya (Nairobi) inamilikiwa na Wakikuyu. Vile vile wakaazi na wamiliki wengi wa mashamba na biashara katika mji wa Nairobi na mtaa wa Kangemi pamoja na maeneo jirani, ni wa asili ya Kikuyu. Ni kutokana na umaarufu wa lugha hii hasa katika mji wa Nairobi na mtaa wa Kangemi ambapo misamiati yake mingi inapatikana katika lugha ya Sheng. Ifuatayo ni mifano ya leksimu za lugha hii jinsi zinavyojidhirisha katika Sheng.

### **Mfano 7**

| <i>Leksimu mkopo</i> | <i>leksimi asili</i> | <i>maana</i> | <i>lugha</i> |
|----------------------|----------------------|--------------|--------------|
| a) Ngiri             | ngiri                | elfu         | kikikuyu     |
| b) Shosh             | cucu                 | nyanya       | kikikuyu     |
| c) Ndonyo            | dunyu                | soko         | kikikuyu     |
| d) Maidhaa           | madhaa               | wakati       | kikikuyu     |
| e) Mukoro            | mukuru               | mzazi        | kikikuyu     |
| f) Morio             | muriu                | rafiki       | kikikuyu     |
| g) Keroro            | kiruru               | pombe        | kikikuyu     |

Lugha ya Sheng ina misamiati mingi kutoka lugha ya Kikuyu. Jambo hili linatokana na sababu kwamba sehemu hii ya Kangemi pamoja na maeno jirani yana wakaazi wengi wenye asili ya Kikuyu kuliko makabila mengine yanayopatikana katika eneo hili. Kati ya jumla ya wakaazi wote wa eneo hili la Kangemi, jamii ya Wakikuyu inamiliki asilimia 41% ya wakaazi wake. Hii ni kulingana na uchanganuzi wa data yetu kutoka kwa chifu wqa mtaa huu wa Kangemi.

#### **2.1.4 Ukopaji na Utohozi: Maneno ya Kifaransa, Kiluhya, na Kidholuo**

Je, Wabaluhya ni kina nani? Wabaluhya ni Wabantuu wanaopatikana katika Afrika ya Mashariki, magharibi mwa nchi ya Kenya. Neno “Baluhya” huwa na maana ya “watu wenye uhusiano wa kiukoo” na hujumuisha watu wanaotoka katika makabila mengi yenye sifa za kifonolojia, kimofolojia na kisemantiki zinazokaribiana. Wabaluhya wengi bado wanashikilia na kuendeleza utamaduni na imani zao za kienyeji, lakini kuna wengine ambao ni Wakristo. Kazi yao kuu ni ukulima. Wanaume wengi Wabaluhya mara nyingi huenda mijini na katika machimbo ya dhahabu kule Kakamega ili kutafuta kazi. (Wagner 1949).

Habari hizi ni za kuaminika kwani mji wa Nairobi una idadi kubwa sana ya Wabaluhya. Inaaminika kwamba wengi wao hufanya kazi mjini Nairobi kama mabawabu na wapishi. Ingawaje mjini Nairobi kuna Wabaluhya wengi, leksimu zao bado hazijaweza kushudiwa sana katika Sheng, mtaani Kangemi. Labda hii inatokana na sababu kwamba jamii ya Wabaluhya ni jamii ambayo inajumuisha lahaja zaidi ya 17 hivi kwamba wakati fulani huwa vigumu kwa wanajamii hawa wote kuwasiliana wanapozungumza. Kwa mfano Kibukusu na Kimaragoli zote ni lahaja za Kibaluhya lakini wanajamii wa lahaja hizi mbili za Kiluhya huwa hawaelewani katika mazungumzo yao.

Kidholuo ni lugha ambayo huzungumzwa na Wajaluo wanaopatikana magharibi mwa nchi ya Kenya. Jamii hii hasa ile inayoishi mjini Nairobi huenzi sana kujihusisha na uzungumzaji wa Kiingereza au lugha yao ya mama (Kidholuo). Uzungumzaji wao wa Kiswahili (kwa wengi wao) huwa wa kiwango cha chini sana hivi kwamba huwa hawazifuati sheria na kanuni za kisarufi ambazo huongoza na kuelekeza matumizi ya Kiwahili. Katika eneo la Kangemi, idadi ya wajaluo

ni ndogo sana ikilinganishwa na ile ya Wakikuyu. Hii ndiyo sababu leksimu za kidholuo bado hazijaweza kushuhudiwa kwa wingi katika Sheng mtaani Kangemi.

Kifaransa ni lugha ambayo kiasili huzungumzwa na Wafaransa, kutoka taifa la Ufaransa. Lugha hii haina mizizi yake katika nchi ya Kenya. Mizizi ya Kifaransa hasa iko katika mataifa yaliyotawaliwa na Ufaransa. Mataifa haya hasa yanapatikana magharibi mwa bara la Afrika. Kenya si mojawapo ya mataifa hayo. Hii ndiyo maana leksimu za Kifaransa hazipatikani mno katika Sheng. Ifuatayo ni mifano ya leksimu za, Kibaluha na kidholuo jinsi zinavyojidhihirisha katika Sheng.

### **Mfano 8**

| <i>Leksimu mkopo</i> | <i>leksimu asili</i> | <i>maana</i> | <i>lugha changizi</i> |
|----------------------|----------------------|--------------|-----------------------|
| a) Sota              | sota                 | kufilisika   | Kiluhya               |
| b) Atoti             | atoti                | msichana     | Kidholuo              |
| c) Saikoro           | msakhulu/saikoro     | mzee         | Kiluhya/Kikisii       |
| d) Buda              | budha                | baba         | Kiswahili/ Kihindi    |

Neno buda limeeleweka na wataalamu kadhaa kama neno la Sheng linalotokana na neno la kihindi “budha,” lenye maana ya mtu mwenye heshima zake au mwanzilishi wa dini ya “Budhism.” Lakini huu sio ukweli wa asilimia mia moja. Ifahamike kwamba lugha ya Kiswahili pia inalimiliki neno hili “buda” lenye maana ya ndovu mzee au mwanamume mzee aliyeanza kung’oka meno. Vile vile, lugha huwa na mazoea ya kukopa kutoka kwa lugha iliyo karibu nayo au yenye sifa zinazokaribiana nayo. Kwa misingi hii kuna uwezekano mkubwa sana kwamba

Sheng ilikopa neno buda kutoka kwa lugha ya Kiswahili wala sio Kihindi. Yaani Kiswahili ki karibu sana na Sheng kuliko Kihindi.

## 2.2 Mbinu ya Ukatizaji.

Ukatizaji ni mbinu ya kuundia maneno ambayo huunda maneno kwa kuyafupisha. Katika mbinu hii vile vile, maneno huundwa kwa kudondosha silabi moja au zaidi, (Jefwa, 2011: 51).Tuki (1990), nayo inasema kuwa: “*ukatizaji ni hatua ya kufupisha neno kwa kuondoa sehemu ya mwanzoni au mwishoni*”. Neno “sehemu” katika fasiri hii ina maana ya “silabi.”

Kulingana na fasiri hizi mbili za neno ukatizaji’ tunapata kuelewa kwamba ukatizaji ni ufupishaji wa neno, katika lugha yoyote ile. Iribemwangi na Mukhwana (2011:166) nao wana maoni kuwa ukatizaji ni mbinu ya uundaji wa maneno inayohusu ufupishaji wa majina, maneno au vifungu vya maneno. Yule (1985:54) naye anasema kwamba ukatizaji hutokea pale ambapo neno lenye zaidi ya silabi moja hupunguzwa silabi ili neno hilo liwe fupi kimuundo. Kulingana na maoni ya wataalamu hawa, ni bayana kwamba jukumu msingi la ukatizaji ni kufupisha silabi fulani za mwanzo, kati au za mwisho wa neno ili kuunda neno jipya. Mbinu hii ya uundaji wa maneno hutumika na lugha nyingi ulimwenguni. Kwa mfano, lugha ya Kiingereza imeunda maneno yafuatayo kwa kutumia mbinu hii.

### Mfano 9

|    | <b>Neno</b> | <b>ukatizaji</b> |
|----|-------------|------------------|
| a) | Professor   | prof             |
| b) | Coka cola   | coke             |

Lugha ya Kiswahili pia huwa na maneno yaliyoundwa kutokana na michakato ya mbinu hii ya ukatizaji. Mifano ya maneno hayo ni pamoja na yafuatayo.

### **Mfano 10**

| <b>Neno</b> | <b>Ufupishaji</b> |
|-------------|-------------------|
| Bibi        | Bi                |
| Mwanamke    | Mke               |
| Mwanamume   | Mume              |
| Bibi harusi | Bi. Harusi        |

Lugha ya Sheng pia inayo maneno yaliyoundwa kwa mbinu hii. Hata hivyo maneno ya Sheng yaliyoundwa kwa mbinu hii huwa ya kukopwa kutoka katika leksimu za lugha zingine. Yaani, lugha hii huwa haina maneno yake binafsi ya asilia ila tu, yale ya kujibunia. Hivyo basi maneno ambayo yamekatizwa katika lugha hii, mwanzoni huwa yamekopwa (na yakatoholewa) kisha yakafupishwa au kukatizwa. Tazama mifano hii ifuatayo:

### **Mfano 11**

| <b>Leksimi mkopo</b> | <b>leksimi asili</b> | <b>maana</b> | <b>lugha changizi</b> |
|----------------------|----------------------|--------------|-----------------------|
| a) Practice          | / tizi:/             | zoezi        | Kiingereza            |
| b) Sister            | / siz /              | dada         | Kiingereza            |
| c) Saturday          | / sato: /            | jumamosi     | Kiingereza            |
| d) Jesus             | / jesi: /            | yesu         | Kiingereza            |
| e) Dereva            | / dere: /            | dereva       | Kiwsahili             |

- |    |            |          |       |            |
|----|------------|----------|-------|------------|
| f) | Brother    | / bro: / | kaka  | Kiingereza |
| g) | Basketball | / bako / | mpira | Kiingereza |

Kati ya maneno yaliyokatizwa kuna yale ambayo hufanyiwa marekebisho ya kifonolojia hivi kwamba matamshi au sauti za maneno hayo hurefushwa yanapotamkwa. Muundo wa pili huwa wa kimofolojia. Yaani neno husika hukatizwa tu lakini maana msingi ya neno hilo huwa haibadiliki. Huddleston (2002: 1634) anasema kuwa kuna aina tatu za ukatizaji; ukatizaji awali, ukatizaji kati na ukatizaji tamati. Kulingana na uchanganuzi wa data yetu tumebaini kwamba lugha ya Sheng inatawaliwa na sifa za ukatizaji awali na tamati. Sifa za ukatizaji wa kati haina. Hivi ndivyo ilivyo katika lugha karibu zote zenye sifa ya kibantu. Lugha hizo huwa na sifa za ukatizaji awali na tamati, na sio ule wa kati. Hivyo basi Sheng pia imechukua sifa hizo za kibantu zinazohusiana na ukatizaji.

### **2.3 Mbinu ya Uambishaji.**

Uambishaji huwa utaratibu wa kuongezea viambishi katika mzizi wa leksimu ili kuunda leksimu mpya. Mbinu hii hujumuisha viambishi awali na viambishi tamati. Viambishi hivi huambishwa kwenye mzizi wa neno ili kuunda maneno mapya. (Jefwa 2010: 52). Matthews (1997:7) naye anasema kuwa uambishaji ni utaratibu wa kuongezea herufi, sauti au makundi yao katika mzizi wa neno na kwamba nyongeza hiyo hubadilisha maana na uamilifu wa neno hilo. Richards na wengine (1985:105) pia wana maoni kwamba uambishaji ni uongezeaji wa viambishi katika mzizi wa neno kwa lengo la kuunda neno jipya.



Sheng huitumia mbinu hii pia ili kujiundia leksimu mpya. Hata hivyo leksimu za Sheng zilizoundwa kwa mbinu hii huwa za mkopo. Leksimu hizo hukopwa kutoka kwa lugha kadhaa kisha hutoholewa kabla ya kufanyiwa uambishaji. Viambishi ambavyo hutumiwa huwa viambishi awali na viambishi tamati.

### **Mfano 12**

| <b>Uambishji (mofu)</b> | <b>Leksimu lekska</b> | <b>Maana</b>           |
|-------------------------|-----------------------|------------------------|
| a) M+ shii              | Mshii                 | Msichana               |
| b) U+ fala              | Ufala                 | Ujinga                 |
| c) U+ sorora + ji       | Usororaji             | Udadisi                |
| d) M + sapere           | Msapere               | Mkikuyu                |
| e) M + ngoso            | Mngoso                | Mzungu                 |
| f) Ki + jadhee          | Kijadhee              | Kidholuo               |
| g) Vi + noma            | Vinoma                | Vibaya                 |
| h) Vi+ dedli            | Videdli               | Hatari                 |
| i) Ku+ nais             | Kunais                | Kufurahisha/ Kupendeza |
| j) Ku+ akt              | Kuakt                 | Kuigiza                |

Katika mifano hii ni bayana kwamba kuna viambishi vya unominishaji vinavyojidhihirisha. Viambishi hivi vinawakilishwa na mofu {m}, {u}, {ki} na {ku} kama zinavyojitokeza kwenye maneno kama vile “msupa,” “kunais” na “usororaji.” Pia mfano huu unajumuisha mofu zinazowakilisha vielezi. Mifano ya mofu hizi ni pamoja na; {vi} kwenye maneno “vinoma” na “videdli.”

## 2.4 Mbinu ya Ubadilishaji Silabi.

Katika mbinu hii ya ujenzi wa maneno, neno kopwa hutoholewa kwanza. Halafu, silabi za neno hilo toholewa hupanguliwa na zikapangwa upya. Upanguaji na upangaji upya wa silabi za neno hilo husika, hulipa neno hilo ujenzi au muundo mpya wa kinyume nyume. Muundo huo mpya huwa haubadilishi maana asilia ya neno hilo. Mbinu hii ya uundaji wa maneno bado haijatia fora sana katika lugha zingine za kitaifa na za kimataifa. Ni jambo gumu kupata lugha nyingine kando na Sheng ikiwa imetumia mbinu hii katika uundaji wa leksimu zake. Hii ni mbinu ya kipekee ambayo jamii ya Sheng inajivunia kuwa nayo ulimwenguni kote. Mbinu hii huifaa jamii hii sana kwa sababu wao pekee yao ndio huitumia katika ufichaji wa siri za mazungumzo yao.

Ogechi (2005:340) anasema kwamba neno husika hukopwa kisha matamshi ya neno hilo hurekebishwa kabla ya silabi za neno hilo kurekebishwa. Ubadilishaji silabi huu huwa utaratibu wa kimakusudi ambao hutumiwa na Sheng kwa kuundia leksimu zake. Ifuatayo ni mifano ya leksimu za Sheng zilizoundwa kwa mbinu hii ya ubadilishaji silabi.

### Mfano 13

| <i>Leksimu changizi</i> | <i>leksimu toholewa</i> | <i>ujenzi kinyume</i> | <i>lugha changizi.</i> |
|-------------------------|-------------------------|-----------------------|------------------------|
| a) Story                | stori                   | risto                 | Kiingereza             |
| b) Card                 | kadi                    | dika                  | Kiingereza             |
| c) Nyumba               | nyumba                  | mbanyu                | Kiswahili              |
| d) Mbele                | mbele                   | lembe                 | Kiswahili              |
| e) Manyanga             | manyanga                | nganya                | Kiswahili              |

Kulingana na mifano hii leksimu changizi ni leksimu ambazo zina uwezo wa kueleweka bayana na mwanajamii wa lugha husika. Lakini punde tu leksimu hizi zinapofanyiwa marekebisho ya ubadilishaji silabi, maana msingi ya neno hilo hufichwa kiasi kwamba huweza kueleweka tu na watu wa jamii lengwa. Maana msingi ya neno hilo huwa haibadiliki. Vile vile maneno ambayo hutumika katika mbinu hii ya uundaji wa maneno huwa ya mkopo.

### **2.5 Onomatopia: Tanakali za Sauti.**

Onomatopia pia hujulikana kama tanakali za sauti. Onomatopia ni ujenzi wa neno kwa kuiga sauti au mlio wa kitu. (TUKI, 2009: 43). Iribemwangi na Mukhwana (2011: 159) nao wana maoni yanayodai kwamba Onomatopea ni mbini ya uundaji leksimu ambapo leksimu huundwa kutokana na sifa, uamilifu, umbo, sauti au milio. Kuna madai mengine yanayosema kwamba Onomatopia ni uundaji wa maneno kutokana na sauti asilia. Lugha nyingi ulimwenguni huwa na sifa ya kujiundia maneno kwa kutumia mbinu hii ya Onomatopia. Kwa mfano, lugha ya Kiingereza ina mifano ifuatayo ya Onomatopia.

| <b>Kiingereza</b> | <b>maana</b>             |
|-------------------|--------------------------|
| Hizz              | pumua kwa sauti ya nyoka |
| Crowl             | enda kwa tumbo           |
| Slither           | enda kama konokoni       |

Lugha ya Kiswahili nayo ina mifano ifuatayo ya Onomatopia;

| <b>Kiswahili</b> | <b>Maana</b>      |
|------------------|-------------------|
| Kifutio          | Kifaa cha kufutia |

|          |   |
|----------|---|
| Patipati | Aina ya kiatu chenye kamba mbili              |
| Pikipiki | Chombo cha usafiri chenye umbo kama baiskeli. |
| Tukutuku | Chombo cha usafiri chenye magurudumu matatu   |

Mifano hii ya Onomatopia za Kiswahili imetokana na sifa zinazotokana na vitenzi husika. Vitenzi hivi ni “fagia” na “futa.” Leksimu “pikipiki” na “patipati” nazo ni Onomatopia zinazotokana na sauti ambazo vifaa hivyo hutoa punde vinapokuwa katika matumizi.

Lugha ya Sheng pia hujiundia leksimu zenye sifa za Onomatopia. Inazo mifano kadha ya maneno yalioundwa kwa mbinu hii. Mifano ya leksimu hizi ni kama ifuatayo.

#### **Mfano 14**

| <i>Leksimu tanakali</i> | <i>Maana</i>  | <i>Lugha</i> |
|-------------------------|---------------|--------------|
| a) Bling bling          | mapambo ghali | Kiingereza   |
| b) Mnga'aro             | mavazi        | Kiswahili    |
| c) Poko                 | kahaba        | Sheng        |
| d) Mburrcha             | matatizo      | Sheng        |

Leksimu za Sheng ambazo huundwa kwa misingi ya mbinu hii huwa chache ikilinganishwa na lugha nyingine. La msingi kueleweka hapa - japo halina umuhimu maalum katika kitengo hiki - ni kwamba De Saussure (1916) alikuwa na mawazo kwamba katika lugha (yoyote ile) huwa hakuna uhusiano wa moja kawa moja kati ya kiashiria na kiashiriwa. Dhana hii ya De Saussure

inaonekana kuzua ukinzani fulani na wazo hili la uundaji wa maneno kwa mbinu ya Onomatopia. Hata hivyo hili sio jambo letu la mjadala katika kiwango hiki.

## **2.6 Upolisemia**

Iribemwangi na Mukhwana (2011:166) wanasema kuwa upolisemia ni kule kuongezea maana kwa maneno yaliyomo katika lugha. Hii ina maana kwamba, neno fulani katika lugha fulani linaweza likapewa maana nyongeza, kando na maana leksika ya neno hilo. Kwa mfano katika Kiswahili neno “mzee” hapo awali lilikuwa na maana moja kuu: mtu mwenye umri unaozidi miaka hamsini hivi. Lakini leo hii neno hili limepanua maana yake hivi kwamba lina maana mpya au mtu mwenye sifa za kihadhi bila ya kujali umri. Lakini kwa kiwango fulani tuligundua kuwa huu sio upolisemia jinsi unavyofasiriwa na Iribemwangi na Mukhwana. Katika kiwango cha Sheng, huu ni ukopaji wa maumbo ya maneno ya Kiswahili, kisha maumbo hayo yanafanywa kuwa leksimu na kupewa maana mpya katika lugha ya Sheng.

Ogechi (2005:343) naye anasema kuwa nomino kopwa katika Sheng hupata upanuzi wa maana kisemantiki. Ogechi anatoa mfano wa neno la Kiswahili “chuo” ambalo maana yake msingi ni masomo ya kiwango cha anuai. Neno hili limekopwa na lugha ya Sheng na likapanuliwa maana yake. Katika lugha hii, chuo ni shule yoyote ile iwe ya msingi, chekechea, anuai au Chuo kikuu. Maneno mengine ambayo yameundwa kwa sifa za upolisemia katika lugha hii ya Sheng ni pamoja na:

## Mfano 15

| <i>Neno</i> | <i>maana asili (Swahili)</i> | <i>maana ziada (Sheng)</i> |
|-------------|------------------------------|----------------------------|
| choma       | kuunguza                     | kuvuta bangi               |
| zidi        | pita kiasi                   | kutembea                   |
| teke        | pigo la nguu                 | haraka                     |
| kaa         | keti                         | jamia                      |

### 2.7 Ubunifu wa Leksimu

Ubunifu wa maneno katika lugha huchochewa na mambo kama vile uvumbuzi wa kisayansi wa vifaa vipya katika jamii. Jambo kama hili litokeapo, basi jamii husika huwa haina budi ila kubuni msamiati wa kutumiwa kwa kutajia vifaa hivyo. Kwa mfano lugha ya Kiswahili ilijibunia misamiati ya vifaa vya kisayansi vilivyovumbuliwa kule marekani na vikashirikishwa kiutenda kazi katika mazingira ya Afrika Mashariki: nchini Kenya. Vifaa hivi ni kama vile tarakilishi, barua pepe, barua meme, kipepesi, mtandao na rununu.

Kulingana na Hartmann na Stork (1972:29) ubunifu ni mchakato au matokeo ya kuunda leksimu mpya kimakusudi kutokana na faridi za kimofolojia zilizopo. Katika jamii, kuna hali inayoweza kuzuka na kuwalazimu wanajamii hiyo husika kubuni msamiati wa kutajia kifaa au hali ambayo ni geni kwao. Laksimu kama hiyo huwa haihuzishwi na ukopaji wala othozi. Mbinu hii huwa na sifa za kuitajirisha lugha husika ndani kwa ndani. Lugha za ulimwengu huwa na sifa hii ya kujibunia maneno ili kuakisi au kuziba pengo fulani la hitaji katika jamii. Kwa mfano lugha ya Kiingereza na Kiswahili imebuni maneno yafuatayo ya kuvitajia vifaa vya kisayansi ambavyo vimevumbuliwa hivi maajuzi.

## Mfano 16

### Kiingereza

### Kiswahili

|              |                 |
|--------------|-----------------|
| Hand set     | simu ya mkononi |
| Mobile phone | rununu          |
| Computer     | tarakilishi     |
| Laptop       | kipakatalishi   |
| Ipad         | aipadi          |

Maneno haya hayakuwemo katika leksimu awali za lugha hizi mbili lakini maadam vifaa hivi vimebuniwa kisayansi hivi karibuni katika jamii hizi mbili, ilibidi jamii hizi zibuni maneno ya kuvitajia vifaa hivi. Maneno haya hayatokani na ukopaji wala utohozi.

Jinsi tulivyosema hapo awali kwamba ubunifu wa leksimu mpya katika jamii husika huchochewa na mabadiliko katika mazingara ya matumizi lugha. Kifaa kipya au hali mpya inapozuka Vile vile lugha ya Sheng hujibunia misamiati ili kuirutubisha lugha hiyo kwa leksimu fokofoko. Ifuatayo ni mifano ya leksimu za Sheng zilizoundwa kwa mbinu ya ubunifu.

## Mifano 17

|    | Leksimu buniwa | maana   |
|----|----------------|---------|
| a) | Mbota          | saa     |
| b) | Ngata          | petroli |
| c) | Dinga          | gari    |
| d) | Mboch          | mjakazi |

|    |           |         |
|----|-----------|---------|
| e) | Ngwai     | bangi   |
| f) | Nangoz    | simu    |
| g) | Tei       | pombe   |
| h) | Mawenzere | makalio |
| i) | Manyura   | kufa    |
| j) | Makagare  | mapumbu |
| k) | Tonji     | mwizi   |
| l) | Karao     | polisi  |
| m) | Kacha     | pingu   |

## 2.8 Akronimu

Katika akronimu herufi au silabi za mwanzo za neno au seti ya maneno hutumika kuundia leksimu nyingine mpya. Akronimu aghalabu huandikwa kwa herufi kubwa na hizo herufi husimamia neno fulani mahususi.

Obuchi na Mukhwana (2010:109) wanasema kuwa akronimu ni utaratibu wa kuunda leksimu kwa kufupisha maneno yanayotumiwa pamoja kwa kuchukua herufi au silabi za mwanzo za maneno hayo. Sehemu za kila neno katika kishazi huchukuliwa na kuunganishwa ili kuunda leksimu moja mpya yenye kusimamia dhana moja. Mbinu hii ina sehemu ya matumizi yake hasa katika lugha ya kiingereza. Mifano ya maneno ya kiingereza ambayo yameundwa kutokana na mbinu hii ni pamoja na;



## **Mfano 18**

| <b>Akronimu</b> | <b>Maana Kamili</b>   |
|-----------------|---|
| NASA            | National Aeronautic And Space Administration                  |
| UNESCO          | United Nations Education Scientific and Cultural Organization |
| UNEP            | United Nations Environmental Program                          |
| KANU            | Kenya African National Union                                  |
| KARI            | Kenya Agricultural Research Institute                         |
| KEFRI           | Kenya Forestry Research Institute                             |

La msingi kueleweka hapa ni kwamba katika akronimu, baada ya kuunda leksimu, leksimu hiyo hutamkwa kama neno moja baada ya mazoea, na wala sio kama herufi moja moja.

Mbinu hii ya uundaji wa maneno bado haijakita katika lugha ya Sheng. Hii ni kwa sababu mbinu hii labda jinsi siku zinavyozidi kusonga ndivyo matumizi yake katika lugha hii yatakapoanza kushuhudiwa.

### **2.9 Kaleki: Tafsiri Mkopo**

Hii pia ni moja wapo ya mbinu za uundaji wa maneno. Katika mbinu hii lugha hukopa na ikatafsiri neno au maneno husika moja kwa moja au neno kwa neno. Kwa mfano, lugha ya kiingereza imetumia mbinu hii ili kujipatia msamiati mwingi kutokana na leksimu za lugha nyinginezo kama vile Kijerumani, Kifaransa na Kihispania. Vile vile Lugha ya Kiswahili imetumia mbinu hii ili kujiundia leksimu. Leksimu hizi zimetokana hasa na maneno ya Kiingereza. Ifuatayo ni mifano ya maneno ya Kiswahili yaliyoundwa (kwa mbinu hii ya kalek) kutokana na maneno ya Kiingereza.

## **Mfano 19**

| <b>Kiingereza</b> | <b>Kiswahili</b>        |
|-------------------|-------------------------|
| Sugar mummy       | mama sukari             |
| Sugar daddy       | baba sukari             |
| United Nations    | umoja wa mataifa        |
| Speech organs     | ala za sauti            |
| Cocktail party    | karamu ya mkia wa jogoo |

Hata hivyo mbinu hii ya uundajiwa maneno huwa na changamoto zake. Changamoto hizi hutokana na maana ambayo huweza kutafsiriwa kutokana na maneno yalioundwa katika lugha pokezi. Yaani maana halisi katika lugha chagizi mara nyingi huwa sio tafsiriwa katika lugha pokezi. Lugha ya Sheng bado haitumii mbinu hii katika uundaji wa maneno yake. Mbinu hii vile vile ni ya kimataifa na hutumikizwa hasa kwa lugha zilizo na chembecheme za umataifa.

### **2.10 Uhulutishaji**

Huu huwa mchakato wa kuunganisha maneno mawili yenye maana tofauti ili kuunda umbo la neno lingine lenye maana tofauti. Yaani mwanzo wa neno fulani (la kwanza) huchukuliwa na kuunganishwa na mwisho au mwanzo wa neno la pili ili kuunda leksimu mpya. Lugha nyingi huwa na maneno yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii ya uhulutishaji. Kwa mfano, lugha ya Kiingereza ina mifano ya maneno yafuatayo.

## **Mfano 20**

| <b>Uhulutishaji</b> |   | <b>Maana</b> |                                 |
|---------------------|---|--------------|---------------------------------|
| Smoke + fog         | = | smog         | mchanganyiko wa ukungu na moshi |
| Gas + alcohol       | = | gasohol      | mchanganyiko wa gesi na pombe   |
| Hotel + motor       | = | motel        | msafara wa magari               |

Mbinu hii ya uundaji wa maneno pia inajitokeza katika lugha ya Kiswahili. Yaani kunayo pia majina ya Kiswahili ambayo yameundwa kwa mbinu hii ya uhulutishaji. Mifano ya majina haya katika lugha ya Kiswahili ni kama ifuatayo;

## **Mfano 21**

|         |   |                          |
|---------|---|--------------------------|
| Chamcha | = | Chakula cha mchana       |
| Chajio  | = | Chakula cha jioni        |
| Ukimwi  | = | Ukosefu wa kinga mwilini |
| Fupaja  | = | Mfupa wa paja            |

Mbinu hii ya uunda wa maneno huwa na sifa zinazokaribiana na zile za akronimu. Hata hivyo hizi ni mbinu mbili tofauti za uundaji wa maneno, jinsi tumevyofafanua katika maelezo ya kila mfano wa uundaji wa maneno kwa misingi ya mbinu hizi mbili. Lugha ya Sheng haina matumizi ya mbinu hii.

## 2.11 Uambatishaji

Kulingana na Franklin na Rodman (1988:137) uambatanishaji ni mbinu ya kuunda maneno kwa kuunganisha maneno mawili ambayo kwa kawaida huwa hayawi pamoja (kwa mujibu wa muundo wa lugha husika) ili kuunda neno jipya. Neno linalojitokeza huwa neno ambatano. Neno hilo jipya huwa halitazamwi kama maneno mawili ila neno moja. Neno ambalo huundwa hivi huwa na maana tofauti na maneno awali ambayo yalitumika katika uundaji wake. Lugha nyingi kama vile kiingereza, Kiswahili na Sheng zimejiundia maneno kwa kutumia mbinu hii. Kwa mfano, leksimu zifuatazo hujitokeza katika lugha ya Kiingereza.

### Mfano 22

|       |   |      |   |           |
|-------|---|------|---|-----------|
| Glass | + | ware | = | glassware |
| Under | + | ware | = | underware |
| Class | + | room | = | classroom |
| Bed   | + | room | = | bedroom   |
| Text  | + | book | = | textbook  |
| House | + | girl | = | housegirl |
| Hand  | + | bag  | = | handbag   |
| Foot  | + | ball | = | football  |

Vile vile mifano ifutayo hujitokeza katika lugha ya Kiswahili.

### Mfano 23

|          |   |       |   |               |
|----------|---|-------|---|---------------|
| Soko     | + | huru  | = | sokohuru      |
| Kiangaza | + | macho | = | kiangazamacho |

|        |          |   |             |
|--------|----------|---|-------------|
| Kiinua | + mgongo | = | kinuamgongo |
| Mwana  | + jeshi  | = | mwanajeshi  |
| Bata   | + mzinga | = | batamzinga  |
| Paka   | + shume  | = | pakashume   |

Katika mifano hii ya Kiingereza na Kiswahili ambayo tumeitaja hapo juu, maneno mawili ya awali ambayo hutumiwa katika uundaji wa neno ambatano, huwa na maana yazo kileksia. Lakini punde tu yanapounganishwa ili kuunda neno jipya (neno ambatano) maneno hayo ya awali hupoteza maana yazo asilia. Neno jipya ambalo huundwa kutokana na maneno hayo mawili huchukua maana leksia iliyo tofauti na maana za maneno ambayo yaliliunda. Sheng pia huwa na maneno ambayo yameundwa kwa misingi ya mbinu hii. Mifano ya maneno haya ni pamoja na mifano ifuatayo;

#### **Mfano 24**

| <b>Uambatishaji</b> |            | <b>maana</b> |
|---------------------|------------|--------------|
| Buu + fee           | = bufee    | nauli        |
| Chiki + dii         | = chikidii | msichana     |

#### **2.12 Unyumbuzi Kapa**

Unyumbuzi kapa huchukuliwa kama aina fulani ya uambishaji, japo ni uambishaji ambao haudhihiriki kimofolojia. Hivyo basi hata ingawa leksimu huwa haiwi na viambishi vya kiothografia huwa inachukuliwa kwamba viambishi hivyo huwa kapa.

Kuhusu unyumbuzi kapa, Katamba (1993:54) ana maoni kwamba leksimu mpya inaweza kuundwa bila ya kubadili umbo la leksimu asilia. Katika mchakato huu leksimu hubadilisha kategoria yake bila kuambishwa wala kufanyiwa jambo lolote linaloweza kubadili umbo la leksimu hiyo. Yaani leksimu ambayo ni nomino inaweza ikatumika kama kitenzi katika mazingira tofautitofauti.

Matumizi ya unyumbuzi kapa katika uundaji wa maneno hujibainisha vyema katika lugha ya kiingereza kuliko lugha ya Kiswahili na Sheng. Mfano ufuatao ni wa Kiingereza. Katika mfano huu leksimu *cook* limetumika kwa maana ya nomino na maana ya kitenzi mtawalia.

### **Mfano: 25**

- a) Agness will cook today (Agness atapika leo)
- b) Agness is the cook today (Agness ndiye mpishi leo)

Katika mfano wa kwanza neno *cook* linajitokeza kama kitenzi na katika mfano wa pili neno *cook* linajitokeza kama nomino. Mbinu hii haikujitokeza katika uchanganuzi wa data yetu. Hii ilitokana na sababu kwamba lugha ya Kiswahili na Sheng ni lugha zenye sifa za lugha za kibantu. Lugha za Kibantu huwa lugha ambishi bainishi. Yaani ili kategoria ya neno ibadilike ni lazima viambishi nyambuzi viongezwe kwenye mzizi wa neno husika.

### **2.13 Ujenzi Ghairi**

Kulingana na Warambo (2011:41) ujenzi ghairi ni hali ambapo leksimu ya aina fulani (mara nyingi huwa ni nomino) inapunguzwa kimaumbo ili kuunda leksimu nyingine yenye umbo

tofauti. Mara nyingi leksimu ambayo huundwa huwa kitenzi. Kwa mfano lugha ya Kiingereza imeunda maneno yafuatayo kwa kutumia mbinu hii ya uundaji wa maneno:

### **Mfano 26**

| <b>Neno awali (nomino)</b> | <b>neni undwa (kitenzi)</b> | <b>maana</b> |
|----------------------------|-----------------------------|--------------|
| Actor                      | act                         | igiza        |
| Driver                     | drive                       | endesha      |
| Televisheni                | televise                    | tangaza      |
| Prayer                     | pray                        | omba         |
| Editors                    | edit                        | Hariri       |
| Conductor                  | conduct                     | ongoza       |

Kiswahili na Sheng ni lugha mbili ambazo zina sifa za kiisimu zinazokaribiana sana. Hii inatokana na sababu kwamba Sheng ni kijilahaja au kimelea cha lugha ya Kiswahili. Hivyo basi mara nyingi sifa za kimuundo zinazopatikana katika Kiswahili, pia hupatikana katika Sheng. Mbinu hii ya uundaji wa maneno kwa kiwango kikubwa bado haijashuhudiwa katika lugha ya Kiswahili. Labda hii ndiyo sababu ambayo kwamba ikafanya mbinu hii kukosa mizizi katika uundaji wa maneno ya Sheng vile vile.

## **Hitimisho**

Katika sura hii tumeshughulikia uundaji wa maneno ya Sheng kwa kuzingatia mbinu za uundaji wa maneno kimofolojia. Mbinu za uundaji wa maneno tulizozichunguza na kuzibaini katika lugha hii ni pamoja na: Ukopaji na Utohozi, Uambatishaji, Upolisemia, Onomatopea na Ubunifu. Hata hivyo tuliweza kubaini kwamba, mhimili mkubwa wa uundaji wa maneno katika lugha hii ya Sheng huwa ukopaji na utohozi. Ukopaji na utohozi huu hasa hutokana na maneno ya Kiswahili, Kikikuyu na Kiingereza. Leksimu zingine zinazotokana na lugha zingine zipo japo si nyingi ikilinganishwa na leksimu zinazotokana na lugha hizo tatu ambazo tumezitaja hapo awali. Katika sura ifuatayo tunajadili njia na nyenzo mbalimbali ambazo wanafunzi wa shule za msingi hujifunza Sheng kutokana nazo. Njia hizo ni pamoja na, wazazi, walimu, ndugu, marafiki na vyombo vya habari.



## SURA YA TATU

### 3.0NYENZO ZA UJIFUNZAJI WA SHENG

Katika sura hii tumeshughulikia mambo kadha wa kadha ambayo kwa hakika huchangia pakubwa katika kuzalisha, kufundishana kukoleza leksimu za Sheng katika akili za wanafunzi hasa wale wa shule za msingi. Ni uraibu huu wa matumizi ya Sheng ambao umechangia na unaedelea kuchangia kuwepo kwa matokeo mabaya ya mitihani ya Kiswahili katika shule za msingi katika eneo hili la kangemi . Inawezekana kwamba zipo sababu nyinginezo za kimsingi ambazo huchangia kuwepo kwa matokeo mabaya ya somo hili. Sababu hizi nyingine hueda zikawa ni pamoja na; umaskini, dawa za kulevya na ukwepaji wa masomo shuleni. Hata hivyo sisi hatukujikita kwa hayo. Badala yake tuliamua kukita katika kigezo cha matumizi ya Sheng kwa sababu tulichokishughulikia ni isimujamii na wala sio sababu za kiuchumi.

Katika utafiti wetu tuliweza kugudua kuwa zipo njia nyingi zenye mvuto wa kipekee ambazo huwachochea wanafunzi wa shule za msingi katika kujifunza Sheng na kisha baadaye wanafunzi hawa wakawa waraibu wa matumizi ya lugha hii ya Sheng, si shuleni tu bali pia katika sehemu nyinginezo zinazopatikana katika jamii. Mifano ya sehemu hizo ni pamoja na; makanisani, nyumbani, masokoni na hata misikitini. Tulipojiuliza swali hili, “je wanafunzi hawa hujifunza Sheng vipina wapi?”. Jibu tulilopata ni kwamba wao hujifunza Sheng kupitia kwa njia zifuatazo: vyombo vya habari, marafiki, ndugu zao, wazazi na pia walimu wao. Huu ndio ukweli ambao data za utafiti wetu zilitudhihirishia.

### **3.1 Vyombo Vya Habari**

Je, vyombo vya habari ni nini? Vyombo vya habari ni vifaa vya mashirika ya utangazaji ambavyo mashirika haya huvitumia ili kuwafikishia ujumbe wasikilizaji wao mbalimbali. Miongoni mwa wasikilizaji hawa huwa vijana kwa wazee. Wengi wa vijana hawa huwa ni wanafunzi wa shule za msingi. Kati ya vipindi ambavyo hutangazwa kupitia kwa vyombo hivi vya habari Vipo vipindi ambavyo hutangazwa kwa kutumia lugha ya Sheng. Sheng huwa na mvuto wa kipikee kwa vijana hawa na vile vile, lugha hii ina ufuasi mkubwa sana miongoni mwa vijana. Yaani vijana hujitambulisha sana kwa kujihusisha na Sheng kuliko lugha nyingine yoyote ile. Ikumbukwe kuwa, Wanafunzi wengi wa shule za msingi huwa wapenzi wa vipindi hivi. Hivyo wao hujaribu sana tena kadri ya uwezo wao ili kuelewa ujumbe unaowasilishwa katika vipindi hivyo kupitia kwa lugha ya Sheng. Iwapo lipo neno la Sheng ambalo hawakulielewa basi wao hujitwika jukumu la kutafuta maana kamili ya leksimu hiyo hasa kwa kuwauliza marafiki na ndugu zao. Kila neno jipya ambalo wao hujifunza huwa leksimu mpya na wao huiongeza katika idadi ya leksimu za Sheng wanazozielewa.

Ikumbukwe kuwa katika vipindi ambavyo hutangazwa kupitia kwenye vyombo vya habari, vipo vipindi kadhaa ambavyo hufundisha misamiati mipya ya Sheng. Mifano ya vyombo hivi hasa huwa vile vya redio.

#### **3.1.1 Redio.**

Redio ni chombo cha habari ambacho huwa na uwezu wa kuwafikia watu wengi sana kwa wakati mmoja. Angalau asilimia 80% ya wananchi kwa jumla humiliki chombo hiki cha utangazaji. Katika eneo la kangemi kila mwanafunzi tuliyemhoji alikiri kwamba wao wanamiliki

redio. Vile vile wapo wanafunzi ambao wazazi wao wamewanunulia simu za mkononi. Simu hizi pia huwa nakitengo cha redio kando na vitengo vingine inavyovijumuishwa. Takribani asilimia hamsini ya wanafunzi wa shule za msingi hutumia vyombo vya usafiri kufika shuleni. Vyombo hivi vya usafiri pia huwa na matumizi ya redio. Hivyo wanafunzi hawa wa shule za msingi wana mawada mapana sana ya kupokea habari kupitia kwa chombo cha habari cha redio. Kati ya habari hizi, zipo habari ambazo huwasilishwa katika lugha ya Sheng.

Utafiti wetu ulitudhihirishia kwamba vipo vyombo vingi sana vya habari ambavyo hutangaza kwa misingi ya Sheng tangia asubuhi hadi jioni. Shirika la utangazaji la Ghetto Redio ndilo shirika lililojibainisha zaidi katika data za utafiti wetu. Shirika hili huwasilisha sana matangazo yake kwa lugha ya Sheng. Mifano mingine ya mashirika ya vyombo vya habari (redio) tulivyovibaini ni pamoja na:

### **Vyombo vya habari vya redio**

- a. Redio jambo
- b. Redio maisha
- c. Ghetto redio
- d. Milele F.M
- e. Kiss F.M
- f. Redio citizen

Hii ni mifano tu ya vyombo vya habari ambavyo hasa hutangaza kwa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, kati ya vipindi ambavyo huwasilishwa katika vyombo hivi vya utangazaji, vipo vipindi

ambavyo huwasilishwa kwa lugha ya Sheng. Vipindi hivyo huambatana na mazungumzo na miziki iliyocharazwa hasa kwa lugha ya Sheng. Mifano ya vipindi hivi ni pamoja na:

**Redio**

**Kipindi**

- |                 |                |
|-----------------|----------------|
| 1. Redio jambo  | Teketeki ..... |
| 2. Ghetto redio | Majambos.....  |
| 3. Redio maisha | Pamoja.....    |

Hii ni baadhi ya mifano ya vyombo vya redio ambavyo vina vipindi viwasilishwavyo kwa lugha ya Sheng . Wawasilishaji wa vipindi hivi huzungumza lugha ya Sheng tena kwa ufasaha wa hali ya juu. Hivyo wawasilishaji hawa huwa mfano mwema wa kuigwa na wanafunzi hawa wa shule za msingi.Vilevile, nyimbo nyingi ambazo huambatana na vipindi hivyo huwa zile ambazo zimeimbwa kwa lugha ya Sheng. Wanafunzi hawa wa shule za msingi huzielewa nyimbo hizo na mara nyingi wao huziimba nyima hizo hata wakiwa mashuleni.

Wanafunzi hawa wa shule za msingi huwa wafuasi wakubwa sana wa wanamuziki hawa ambao huimba kwa lugha hii ya Sheng. Mifano ya wanamuziki hawa tuliawatambua kutokana na data zetu ni pamoja na:

1. Redsun
2. Ecodyda
3. Octopizzo
4. Nameless
5. Wahuu

*(Hawa wanamuziki tulipata kuwabaini kutokana na data za utafiti wetu)*

### 3.1.2 Televisheni.

Televisheni ni chombo cha habari ambacho huwasilisha matangazo yake kupitia kwa mawimbi ambayo hufanikisha uwasilishaji wa picha ambazo huambatana na sauti (oxford advanced learners Dictionary 8<sup>th</sup> edition). Chombo hiki cha utangazaji hupendwa sana na wasikilizaji wengi wakiwemo wanafunzi wa shule za msingi. Wao hukipenda chombo hiki cha utangazaji kuliko kile cha radio. Hali hii inatokana na sababu kwamba chombo hiki huweza kusikilizwa na vile vile kutazamwa kwa wakati mmoja. Hivyo, kama ni wimbo unaoimbwa mtazamaji huweza kusikia anayoyasema mwimbaji pamoja na jinsi anavyojidhihirisha runingani.

Hivyo hali hii huendeleza ukuzaji na ukolezaji wa matumizi ya Sheng katika mazingira ya mwanafunzi. Kwa misingi hii, mwanafunzi huwa hana budi ila kujifunza lugha hii ili aweze kuwiana vyema na mazingira yake. Mwishowe matokeo ya matumizi ya lugha hii huwa si mazuri kwa wanafunzi husika. Masomo yao hasa somo la Kiswahili huathirika pakubwa .

Miongoni mwa vyombo vya habari vilivyojitokeza katika data za utafiti wetu ni pamoja na:

- i. Citizen TV
- ii. NTV
- iii. KTN
- iv. KBC
- v. K24
- vi. KISS TV
- vii. QTV
- viii. U TV

*(Hii ni mifano ya vyombo vya habari vya televisheni jinsi vilivyojitokeza katika data zetu).*

Vile vile data zetu zilitubainishia kwamba vipo vyombo vya televisheni ambavyo hurusha matangazo hayo kupitia kwa mawimbi ya kisasa ya kidijitali. Mifano ya vyombo vya televisheni vinavyotangaza kwa mawimbi haya ya kisasa ni pamoja na:

- i. E TV
- ii. Heritage TV
- iii. Youth TV

*(Hii ni Mifano ya vyombo vya habari hurusha matangazo yao kupitia kwa mawimbi ya kisasa ya kidijitali).*

Katika vyombo hivi vya habari, vipo vipindi ambavyo huwasilishwa kwa lugha ya Sheng. Wawasilishi wa vipindi hivi vile vile huizungumza lugha ya Sheng kwa viwango fulani. Wao huizungumza Sheng kwa ufasaha na kwa mvuto sana. Hivyo wanafunzi wetu hupata kuwaiga na baada ya kuwaiga, wao huyaweka walioyaiga katika utendakazi hasa pale wanapozungumza na wanafunzi wenzao, wazazi wao, waalimu wao na hata ndungu zao. Zoa hili huwa haliishii hapa tu bali huendelezwa hadi katika masomo yao hasa katika somo la uandishi wa insha.

Mifano ya vipindi tulivyovibaini ambavyo huwasilishwa katika lugha ya Sheng katika vyombo hivi vya habari ni pamoja na:

| <b>Kipindi</b> | <b>Televisheni</b> |
|----------------|--------------------|
|                | KISS TV Praizes    |
|                | KTN Tukuza         |
|                | NTV Gospel Hour    |
|                | KBC Sunday Mix     |
|                | Citizen Kubamba    |

Mifano hii ya vyombo vya Televisheni pamoja na vipindi vya televisheni ambavyo hutangaza na kucheza nyimbo za Sheng inatudhihirishia bayana kwamba wanafunzi wa shule za msingi huwa na jukwaa kubwa sana la kujifunza na kuzungumza Sheng. Hatimaye huwa ni athari hasi za uzungumzaji wa lugha hii ambazo hujithiirisha katika matokeo mabaya ya mitihani ya wanafunzi hawa.

### **3.2 Wazazi.**

Utafiti wetu vile vile ulitubainishia kwamba wanafunzi wa shule za msing hujifunza Sheng kupitia kwa baadhi ya wazazi wao. Hawa kwa kawaida huwa ni wale wazazi wachanga ambao umri wao bado haujasonga vile. Yaani wazazi ambao wako kati ya miaka 25 hadi 45. Hapo awali tulisema kwamba Sheng huwa lugha ya vijana. Vijana hawa ni wale vijana ambao hasa huishi na kuendeleza majukumu yao ya kila siku jijini Nairobi, na hasa katika mtaa wa Kangemi. Hivyo wazazi ambao wako katika kategoria hii ya kiumri, bado ni vijana na baadhi yao bado huwasiliana na wenzao kwa kutumia lugha hii ya Sheng. Hali hii huendelezwa na wazazi hawa si makazini kwao tu bali pia viamboni pao. Hapa, wao huwazungumzia watoto wao kwa kutumia lugha ya Sheng. Watoto hawa nao huiga mazungumzo hayo ya wazazi wao. Uigaji huu baadaye huwekwa katika utenda kazi hasa pale wanapozungumza kwa kujibizana na hao wazazi wao. Hatimaye, Sheng hutumiwa na wanafunzi hawa nyumbani pamoja na hata shuleni pao. Kwao wanafunzi hawa, Sheng huwa lugha yao ya mawasiliano, si nyumbani tu bali hata shuleni. Ufuatoa ni mfano wa mawasiliano kati ya mwanafunzi na mzazi wake katika lugha ya Sheng. Mfano huu ulijibaini katika data za utafiti wetu.

## **Mfano 27 Sheng**

*Mzazi: Jose! Ukimaliza kudema iyo sembe, run kwa shop ubai milk na bredi ya kumanga kesho mamoning.*

*Mtoto : Ni fiti dadi!*

## **Tafsiri**

*Mzazi: Joseph! Ukimaliza kula huo ugali, kimbia dukani ili ununue maziwa na mkate wa kula kesho asubuhi.*

*Mtoto: Ni sawa baba!*

*Mzazi: kim ! Ati mzae wa Atis ameenda majuu?*

*Mwanafunzi: Ndio buda. Alienda jana, najua atanimbaiya nangos huko.*

*Mzazi: Kimani!Ati mzazi wa Atieno ameenda ulaya?*

*Mwanafunzi: Ndo baba.Alienda jana ,najua ataninunulia simu huko..*

Mfano huu ulitubainishia mambo muhimu yafuatayo:

1. Kwamba, wazazi huwa hawaoni tatizo lolote lile pale wanapowanzungumzia watoto wao kwa kutumia lugha ya Sheng. Hivyo, kama lipo kosa, basi kosa hilo litasahihishwa na mwalimu.
2. Kuwa, wanafunzi huwa hawaoni jambo lolote lile lisilo la kawaida pale wazazi wao wanapowazungumzia kwa kutumia lugha ya Sheng. Kwa kufanya vile, wazazi hawa huwathahirishia watoto wao kuwa wao si mafala.



Jambo la msing ambalo makundi haya mawili huwa yanasahau ni kwamba, ingawaje Sheng huweza kufanikisha mawasiliano, lugha hii si lugha inayotambuliwa na serikali au na ngazi yoyote ile ya kielimu. Hiyvo lugha hii haiwezi ikatahiniwa wala ikatumiwa kama lugha ya kupitishia ujumbe wa kielimu mashuleni. Wazazi hawa wanasahau kuwa Sheng huyaathiri matokeo ya watoto wao mashuleni. Wanafunzi wao pia kwa upande mwingine wanaonekana kutofahamu athari za lugha hii hasa katika matokeo ya masomo yao.

### **3.3Walimu.**

Mwalimu ni mwanataaluma ambaye taaluma yake hutegemea ufundishaji wa wanafunzi wake. Riziki ya mwalimu hutegemea ufundishaji. Hivyo jamii humchukulia mwalimu kuwa chemichemi ya busara, hekima na maarifa katika jamii. Shuleni mwalimu huwa nguzo muhimu sana ya elimu kwa wanafunzi wake. Wao humwona mwalimu kama mzazi wa pili na mfano mwema wa kuigwa katika jamii. Hivyo kwa kiasi kikubwa, kila atendalo na kila alifanyalo mwalimu, huwa sawa machoni pa wanafunzi wake. Pamoja na ukweli huu, ipo athari ambayo tayari imeanza kujipenyeza na hatimaye kujiundia makao katika mazingira ya mwanafunzi kupitia kwa mwalimu wake. Athari hii ni lugha ya Sheng, lugha ambayo mwanafunzi hasa wa shule ya msingi sasa ameanza kuipokea na kuitumia kupitia kwa elimu ya mwalimu wake. Swali ni je, walimu hawa wamefaulu vipi kuijua na kuitumia lugha ya Sheng?

Jibu la swali hili ni wazi. Wengi wa walimu wanaohitimu masomo ya shule za upili na kujiunga na vyuo vya walimu ni vijana.

Walimu hawa vijana walipokuwa katika shule za msingi, waliizungumza Sheng. Walipohitimu kujiunga na shule ya upili, huko waliizungumza Sheng. Na vile vile walipojiunga na vyuo vya

ualimu waliizunguza Sheng huko. Hivyo, tayari mazoea ya kuizungumza Sheng yapo na yamekuwa sehemu yao. Walimu hawa bado huwa vijana wanapoanza majukumu yao ya kuwafunza wanafunzi wa shule hizi za msingi. Hivyo mara kwa mara wao hujikuta wakizungumza Sheng kwa kujua au kwa kutojua. Uzungumzaji huu hutendeka wanapokuwa shuleni na hasa madarasani. Utafiti wetu ulitubainishia kwamba walimu hawa ambao wangali vijana, mara kadhaa hujipata wakiyajibu maswali ya wanafunzi wao kwa kutumia Sheng. Hali hii hutokea hasa pale mwanafunzi husika humuuliza mwalimu husika swali kwa kutumia Sheng. Baadaye, huyo mwanafunzi hujenga mazoea ya kuzungumzia mwalimu huyo wao kwa kutumia lugha ya Sheng. Hapo jambo ambalo husahaulika ni kwamba, Sheng si Kiswahili sanifu. Hivyo matumizi yake yanastahili kuekewa mipaka ili mipaka hii isije kuoanishwa na shughuli za lugha ya mawasiliano katika mazingira ya darasani.

Sera za elimu zinadai kwamba ni vyema mwalimu ashuke ngazi hadi afikie kiwango cha uelewa wa mwanafunzi wake ndiposa apate kumwelewa na kumsaidia vyema. Ingawaje jambo hili ni muhali, ni vyema pia kwake mwalimu kufahamu kuwa punde anaposhuka ngazi. Huweza kumuelewa mwanafunzi wake vyema, asije akasahau majukumu yake ya kimsingi kama mwalimu. Jukumu la msingi la mwalimu ni kumuongoza mwanafunzi wake katika taratibu msingi za kielimu kama zinavyofafanuliwa na idara za elimu. Mawasiliano na mazungumzo kwa lugha ya sheng si mojawapo ya taratibu hizi. Ufuatao ni mfano wa mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi wake. Mawasiliano haya yalifanyika katika lugha ya Sheng kama tulivyobaini kutokana na data za utafiti wetu.

**Mf. 28 Mwanafunzi:**

*Sheng: Ticha chali akiwa juu ya madre alafu amdandie mbus, anaweza akapata bol?*

**Mwalimu:**

*Sheng: kwani? Atapata bol tenaipoa sana.*

**Mwanafunzi**

*Tafsiri: Mwalimu mvulana akiwa amemeza dawa za kulevya kisha ambake msichna, je anaweza akapata mimba*

**Mwalimu**

*Kwa nini asipate? Atapata mimba vizuri sana.*

*Mwanafunzi: Mode hii mao jo siitatusidisha?*

*Maze afhali tusare.*

*Mwalimu: Ah msikonde nitawasho.*

*Tafsiri*

*Mwanafunzi: Mwalimu hii hesabu ni ngumu itatuua, heri tuiache*

*Mwalimu: Msiwe wasiwasi nitawaelekeza.*

Mazungumzo haya kati ya mwalimu na mwanafunzi wake ni dhihirisho kamili kwamba mwalimu na mwanafunzi wake walielewana vizuri. Mazungumzo haya yalifanyika darasani wakati wa kipindi cha somo la sayansi. Mada iliyokuwa ikizungumzwa ilikuwa “Dawa za kulevya.” Mazungumzo haya yanatufahamisha vyema kuwa walimu kadhaa huijua lugha ya Sheng na huwasiliana fika na wanafunzi wao madarasani.

Hivyo wanafunzi hawa huweza kujifunza leksimu za Sheng za kisasa na zile za zamani kupitia kwa walimu wao. Leksimu hizi hujidhihirisha vyema katika insha za wanafunzi wao jinsi tutakavyoona hapo baadaye.

### **3.4 Ndugu.**

Wanafunzi wa shule za msingi vile vile hujifunza Sheng kupitia kwa ndugu na jamaa zao. Ndugu na jamaa za wanafunzi hawa huwa na ufasaha wa lugha ya Sheng. Kati yao kuna wale ambao bado wako katika shule za upili, vyuo na vyuo vikuu. Hivyo ndugu za wanafunzi hawa wanapokutana, lugha ya mawasiliano ambayo wao hutumia kwa kiwango kikubwa, huwa lugha ya Sheng. Kwa kufanya hivi, wanafunzi hawa huendelea na kuikuza misamiati ya Sheng wanayoilewa. Umilisi na matumizi ya lugha hii huendelea kuwakolea.

Baadhi ya misamiati ambayo wanafunzi hawa hujifunza kutoka kwa ndugu zao ni pamoja na leksimu za kutaja:

- i. Mavazi
- ii. Misimu
- iii. Masomo
- iv. watu kwa kuzingatia jinsia zao
- v. Magari
- vi. Mataifa
- vii. Taaluma
- viii. Vyakula
- ix. Nyakati

Leksimu za Sheng ambazo wanafunzi hawa hujifunza kutokana na ndugu na jamaa zao ni kama zifuatazo:

**Kikoa**

**Leksimu**

- |            |                            |
|------------|----------------------------|
| 1. Mavazi  | Njuta/jinare/tisho/ngodha  |
| 2. Masomo  | Sayo/mao/kiswa/engo        |
| 3. Watu    | chali/dem/manzi/kuzo/dingo |
| 4. Magari  | nganya/dinga/moti          |
| 5. Mataifa | majuu/yujii/amero          |
| 6. Taaluma | udijo/konkodi/dingo/mboch  |
| 7. Vyakula | mcheti/sembe/nyake/chipo   |
| 8. Nyakati | mamoning/ngware/chee/njeve |
| 9. Miji    | nai/momba/umo/ungem/kibich |

**Tafsiri**

**Kikoa**

**Leksimu**

- |         |                                     |
|---------|-------------------------------------|
| Mavazi  | viatu/jeans/tisheti/chupi           |
| Masomo  | sayansi/hesabu/kiswahili/kiingereza |
| Watu    | mvulana/msichana/mkoi/utingo        |
| Magari  | daladala/gari/gari                  |
| Taaluma | mwalimu/makanga/mwizi/kijakazi      |
| Vyakula | mchele/ugali/nyama/vibanzi          |
| Mataifa | ng'ambo/uganda/marekani             |

Nyakati: asubuhi/alfajiri/macheo/kipupwe  
Miji Nairobi/Mombasa/Umoja/Kangemi/Kibera

*(Hii ndiyo mifano ya leksimu za Sheng iliojitokeza katika hojaji ya utafiti wetu.)*

mifano hii ni ushahidi tosha kwamba wanafunzi wa shule za msingi hujifunza Sheng kutoka kwa ndugu zao iwe ni nyumbani, shuleni au popote pale. Katika utafiti wetu, tuliweza pia kupata mifano ya sentensi za Sheng. Sentensi hizi zilitubaininshia kwamba ndugu hawa huzungumza na kuwasiliana na ndugu zao - ambao ni wanafunzi - kwa kutumia Sheng.

Mifano ya sentensi hizo ni kama ifuatayo:

### **Mfano 29**

*Sheng: Manze bro joo! Ngodha yangu inamis. Umeicheki?*

*jibu: Du! Si uchapilie hiyo ya mbuyu!*

*Tafsiri: Haki samahani kaka! Chupi yangu.*

*Jibu: la! si uvalie hiyo ya baba!*

*Sheng : Kwa nni watoi hawa wanamawari bigi?*

*Jibu: haya si buda wao alimanyula.*

*Tafsiri : lwanini watoto hawa wanateseka*

*Jibu : haya si baba yao alifariki.*

Mifano hii ya sentensi inaonyesha kwamba mawasiliano yaliweza kufanikishwa kati ya wahusika wote wawili. Hii ni kwa sababu muhusika wa kwanza alimuuliza muhusika wa pili

swali naye mhusika wa pili akamjibu. Hivyo, mawasiliano yalitendeka kati yao. Vilevile kutokana na mifano hii ya sentensi, tunapata kuelewa kwamba ndugu wakubwa huwazungumzia ndugu zao wadogo hasaa kwa kutumia lugha ya Sheng. Hivyo ndugu zao wadogo huwa hawana budi ila kuwajibu au kujibiza mazungumzo husika kwa lugha ya Sheng.

### **3.5 Wanafunzi.**

Kutokana na utafiti wetu, tulibaini kwamba wapo wanafunzi ambao hujifunza Sheng kupitia kwa wanafunzi wenzao. Sheleni huwepo wanafunzi ambao tayari huwa wameshabobea katika uzungumzaji wa lugha hii ya Sheng. Wao huwa na misamiati komavu. Mara nying wanafunzi kama hawa hupenda sana kuwasiliana na wanafunzi wenzao kwa kutumia lugha hii ya sheng. Vile vile, hapo shule wapo wanafunzi ambao kwao, lugha ya Sheng huwa ni lugha geni. Misamiati ya Sheng ambayo wao hujua huwa ni michache sana. Hivyo, kwa wanafunzi kama hawa kuzungumza kwa ufasaha kwa kutumia lugha ya Sheng huwatatiza tena sana hapo mwamzoni. Lakini mambo huwa hayasalii kuwa hivi daima. Mambo huanza kubadilika pale wanapoanza kuingiliana kimazungumzo na hao wanafunzi wengine ambao tayari huwa wamebobea katika uzungumzaji wa lugha hii.

Ni baada ya maingiliano haya ambapo asilimia 70% ya wanafunzi wa shule za msingi katika eneo bunge hili la kangemi huwa na uwezo wa kuelewa na kuzungumza kwa lugha ya Sheng. Hivyo, asilimia hii ya wanafunzi tayari huwa imetumbukia katika athari za kutofanya vyema katika mitihani yao ya somo la kiswahili. Katika utafiti wetu, tuliweza kubaini mifano kadha ya sentensi za Sheng ambazo hutumiwa na wanafunzi ambao bado huwa hawajabobea sana katika

uzungumzaji wa Sheng. Leksimu zao za Sheng bado huwa hafifu sana. Wakati mwingi wao hutumia leksimu za Sheng zilizokuwa zikitumiwa hapo mwanzo. Tazama mifano ifuatayo:

### **Mfano 30**

*Sheng ya awali: 1 caro, techa wa mao amededi!*

Baadaye wanafunzi hawa huanza kubobea katika uzungumzaji wa Sheng kwa kutumia misamiati ya kisasa. Tazama mfano huu:

*Sheng ya kisasa: Caro! Udijo wa mao amemanyulia!*

Kutokana na uchanganuzi wetu wa data tulizozipokea, ni bayana kwamba, asilimia 62.35 ya wanafunzi wa eneo bunge hili la Kangemi huishia kutofanya vizuri katika mitihani yao ya somo la Kiwahili kutokana na sababu msingi za Sheng. Kwa kawaida, Sheng huwa lugha ya mkato. Ni lugha ambayo hujaribu sana kurahihisha mawasiliano miongoni au kati ya wazungumzaji husika. Hivyo, mazoea haya huendelezwa na wanafunzi hawa mashuleni na hata katika somo la uandishi wa insha. Ni hali hii ambayo huwafanya wanafunzi hawa kutofanya vizuri katika uandishi wa insha na kujibu maswali ya ufahamu.

Katika sura inayofuatia, tunaenda kuangalia kwa kuchanganua uandishi wa insha za wanafunzi hawa pamoja na matokeo ya mitihani yao ya somo la Kiswahili. Uchanganuzi wetu ulilenga matokeo ya mitihani ya Kiwahili kwa mfululizo wa miaka mitatu iliyopita.



## SURA YA NNE

### 4.0 UCHANGANUZI WA DATA ZA MATOKEO YA MITIHANI

Katika sura ya tatu tulitathmini vianzo mbali mbali ambavyo wanafunzi wa shule za msingi hujifunza Sheng kutokana navyo. Vianzo hivyo tulivyojadili ni pamoja na walimu, wazazi, ndugu, wanafunzi, na mashirika ya utangazaji kupitia kwa vyombo vya habari kama vile redio na televisheni.

Katika sura hii ya nne tunaenda kujadili kwa kuchanganua insha za wanafunzi wa shule kadhaa za msingi. Lengo letu hapa lilikuwa ni kuona kama kweli istilahi za Sheng hujithirisha katika tungo za wanafunzi hawa. Data za utafiti wetu kuwa jambo hili ni la kweli. Tungo kadha tulizozichanganua zilidhibitisha haya kuwa ya kweli. Hivyo, katika vielelezo vya insha vifuatavyo, tunaenda kuchanganua kwa kuthirisha jinsi ambavyo matumizi ya Sheng yamekuwa sehemu msingi ya tungo za wanafunzi hawa. Hivyo basi, ni kuwepo kwa istilahi hizi za Sheng katika insha ambako kunawafanya wanafunzi hawa kutofanya vizuri katika uandishi wa insha za mitihani yao ya kitaifa.

### 4.1 Kielelezo Cha Kwanza Cha Insha: Sheng

#### **MADA YA INSHA: ASIYESIKIA LA MKUU HUVUNJIKA MKUU.**

*Ama kweli, wazeia wa kitambo hawakutuvako waliposey eti asiyesikia la mkuu hufikwa na makuu. Methali hii ilifichuka wazi baada ya kamdenge kingine cha mtaa kujuta maishani. Hivi ndivyo risto yake alikuwa na kutokelezea.*

*Hako kadem kaliishi uko ocha. Keja yao ilikuwa ngori tu sana. Mukoro wake muhastuler mbaya mbovu masake alikuwa amechapa tu samna. Fadhee naye? Wacha! Hata hityo tusiguzie. Nayeye je? Alikuwa mtotois yaani toto si toto!*

*Huko chuo kulikuwa ngori kuzidi. Mamode wake walimpiga mamboko ungalithink alikuwa punda anayefosiwa kubeba magoods mob tu sana. Mabeste wake naao, walimpara atumie machoves. Form nazo? Walikuwa walembe kufika. Odijos walimkazia astop madre kuishia lakini aliwatupia mikono akisema Izeni jo, laif nikujibamba joo!*

*Machali walimvako na kumchocha hadi akaingia box. Alidarwa hadi akadarika. Day moja, alipewa machoves hadi akalewa kuruka.*

*Manze jo? Kidame kilimangwa kikamangika. Mwishowe, aliget boll. Hapo ndipo alishikanisha waya inayobonga kuwa asiyesikia ya watunguyas hujuta.*

#### **4.1.1 Tafsiri Ya Kielelezo Cha Kwanza Cha Insha**

*Ama kwa kweli wazee wa kitambo hawakutudanganya waliposema kuwa asiyesikia lamkuu huvunjika guu. Methali hii ilifichuka wazi baada ya kisichana kimoja cha mtaani kujuta maishani. Hivi ndivyo habari zake zilianza na baadaye zikazagaa.*

*Hicho kisichana kiliishi huko mashambani. Nyumba yao ilikuwa imechakaa. Wazazi wake walikuwa maskini wa mwisho. Mama yake alikuwa amekonda sana. Baba yake naye, hayo hayawezeki. Yeye mwenyewe alikuwa mrembo sana. Urembo wake haukuwa na kifani.*

*Huko shuleni mambo yalikuwa mabaya sana. Walimu wake walikuwa wakimpiga viboko kama punda aliyekuwa akilazimishwa kubeba mizigo mizitosana.*

*Rafiki zake nao walimwasi atumie dawa za kulevya. Maisha yao yalikuwa ya hali ya juu. Hakuna mwana aliyewapiki kwa hela na kwa usafi. Walimu walimwonya awachane na matumizi ya dawa za kulevya lakini aliwatupia mkono na kusema, “tulieni, maisha ni burudani au sio!”.*

*Wavulana walimdanganya na kumshawishi hadi akakubali maneno yao. Alidarwa hadi akadarika. Siku moja alipewa dawa za kulevya akalewa kiwango cha kutojielewa*

*La haula! Kisichana kile kilibakwa hadi kikabakika. Mwishowe kisichana kile kilipata mimba.*

*Hapo ndipo aligudua kuwa asiyesikia la mkuu huvunjika guu.*

Mtungo huu ulijitokeza katika data za utafiti wetu. Kulingana na uchanganuzi wetu, mwanafunzi aliyeandika insha hii ni kati ya wanafunzi wale ambao kwa hakika, wameboba katika uzungumzaji wa Sheng. Sababu ya madai haya ni kwamba, insha hii imesheheni misamiati mingi sana ya Sheng. Misamiati hii sio ya mwanafunzi ambaye ameanza kujifunza Sheng hivi karibuni. Hivyo, ingawaje mwanafunzi huyu amelenga maudhui husika vyema, kasoro yake iko katika matumizi ya msamiati. Msamiati anaoutumia si msamiati wa Kiswahili sanifu. Sarufi yake ameichafua kwa misamiati ya Sheng.

Kifuatacho sasa ni kielelezo cha insha nyingine jinsi ilivyojitokeza katika data za utafiti wetu. Kielelezo hiki pia kimesheheni misamiati ya Sheng ila misamiati yake sio ya kiwango cha juu kama ile ya kielelezo cha kwanza.

## 4.2 Kielelezo Cha Pili Cha Insha: Sheng

### MADA: ASIYESIKIA LA MKUU HUFIKWA NA MAKUU.

*Ama kweli wazee na waiya hawakutupaka mafuta mgongoni waliponena kuwa asiyesikia la mkuu hufikwa na makuu. Maana ya methali hii ilifichuliwa vyema kwa maisha ya chali mmoja aliyeitwa Brusly.*

*Katika ushags ya siaya kuliishi boy mmoja alietwa Brusly. Alikuwa hapendi kuenda chuo. Alikuwa na mabeshte ambao walipenda kumsifu tu sana. Alijidai na kujikamba kuwa yeye ndiye anayejua kila kitu. Kila mara matokeo ya egzam ilipotokea alikuwa danda yaani mayai mbichi Alisahau fika, poa ikizidi kuwa poa huwa si poa net.*

*Day moja, Brusly alizidi klab na kumwona kadem kengine ambako kalikuwa kamebeba mahaga na shep poa. Huyo dem alijiona ako juu tu sana kwa vile ye ndiye alikuwa msupa. Brusly alimuendea yule dem akiwa anabauns. Walibonga pamoja na baada ya siku kinde dem alipatikana ako na boll.*

*Kuisha yeye! Dem alianza kurigret kwa nini akusikia mawaidha ya paro zake. Paro zake walikasirika kwa siku mob lakini uchungu wa mwana ajuaye wavyele.*

*Wavyele wake waliamua kumsaidia na doo na kila kitu na wakaishi vyema baadaye. Alikuwa anaachia masa yake mtoi na kwenda kusel nyanya, vitungu na dania kwa shilling mbao tu.*

*Alishoiwa na boi mmoja kuwa anamdai na wakafunga ndoa na kwanzia hiyo siku alijua kuwa asiyesikia la mkuu hufikwa na makuu.*

#### **4.2.1 Tafsiri Ya Kielelezo Cha Insha Ya 2**

*Ama kwa kweli wazee na wavyele hawakutupaka mafuta kwenye mgongo wa chupa waliponena kuwa asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Maana ya methali hii ilifichuka vyema katika maisha ya mvulana mmoja aliyeitwa Brusly.*

*Huko mashambani Siaya, kuliishi mvulana mmoja aliyeitwa Brusly. Alikuwa hapendi kuhudhuria masomo. Shuleni alikuwa na marafiki ambao walipenda kumsifu sana. Alijidai na kujigamba kuwa yeye ndiye aliyejua kila kitu. Kila mara matokeo ya mitihani yalipotoka yeye ndiye alikuwa wa mwisho. Alisahau kuwa tamu ikizidi utamu huwa si tamu tena.*

*Siku moja Brusly alienda kwenye baa na akakiona kisichana kilichokuwa kimenona makalio sana na chenye maumbile mazuri. Huyu msichana alijiona akiwa mzuri sana kwa jinzi alivyokuwa mrembo. Brusly alimwendea yule msichana akiwa anajisikia kweli kweli.*


*Waliongea pamoja na baada ya siku kumi msichana yule alipatikana akiwa na mimba.*

*Hapo mambo yake sasa yalikuwa yamekwisha!. Msichana yule alianza, kujuta ni kwa nini hakisikiliza mawaidha mazuri ya wazazi wake. Wazazi wake waliudhika kwa siku nyingi lakini uchungu wa mwana ajuaye ni mzazi. Wavyele wake waliamua kumsaidia kwa pesa na mahitaji memgine. Baadaye waliishi vyema kama familia. Alikuwa akimwachia mama yake mtoto kisha anaenda kuuza nyanya, vitunguu na dania kwa shilingi ishirini tu. Baadaye mvulana mmoja alimwambia kuwa alimpenda. Alimwambia kuwa alitaka kumwoa. Baadaye walioana. Tangu siku hiyo, alijua kuwa asiyesikia la mkuu hufikwa na makuu*

Kutokana na uchanganuzi wa kielelezo hiki cha pili, tunapata kuona kuwa, mwanafunzi huyu bado hajaathirika sana kwa misamiati ya Sheng ikilinganishwa na yule mwanafunzi wa kwanza. Misamiati yake ya Sheng ingali ya kiwango cha chini. Hata hivyo, ni bayana kwamba mwanafunzi huyu anao uwezo wa kuwasiliana kwa misingi ya Sheng. Huu ndio ukweli unaodhihirika katika mtungo huu. Ukweli mwengine unaodhihirika ni kwamba, wanafunzi hawa wote wawili wamo katika hatari ya kutofanya vizuri katika mitihani yao ya Kiswahili. Iwapo insha zao za mtihani wa kitaifa zitajumuisha misamiati hii ya Sheng, basi alama watakazozipata katika somo hili hazitakuwa nzuri. Kwa kawaida, alama za insha hujumuishwa na zile za lugha. Hivyo, alama za insha zisipokuwa nzuri basi zitaziathiri zile za lugha. Matokeo yake yatakuwa kwamba, wanafunzi hawa hawatafanya vyema katika somo la Kiwahili.

Ufuatao sasa ni uchanganuzi wa matokeo ya somo la Kiswahili katika shule nne za msingi tulizozitathmini. Shule hizi ni pamoja na: Shule ya Msingi ya kihumbuini, Shule ya Msingi ya Kabete Vet., Shule ya Msingi ya Kangemi na Shule ya Msingi ya New Kihumbuini.

***SHULE YA MSINGI YA KIHUMBUINI: MATOKEO YA MTIHANI WA MWIGO;  
2011 – 2013***




Uchanganuzi huu unaonyesha bayana kwamba wanafunzi wa shule hii ya msingi ya kihumburi hawajakuwa wakifanya vyema katika mitihani yao ya kiswahili kwa jumla. Tatizo lao kuu limekita katika uandishi wa insha. Katika eneo hili wanafunzi hawa wamekuwa wakifanya vyema sa jinsi matokeo yanavyodhihirisha. Mnamo mwaka awa 2011, wanafunzi hawa walipata asilimia 15.44% katika mtihani wa insha. Hii ina maana kwamba wote kwa jumla walianguka mtihani. Mnamo mwaka wa 2012, wanafunzi hawa walipata alama ya 14.13% katika mtihani wa insha. Hii ikiwa na maana kwamba wanafunzi hawa walishuka kwa alama moja ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Mnamo mwaka wa 2013 wanafunzi hawa walipata alama 16.56% katika mtihani wao wa insha. Ingawaje wanafunzi hawa waliimarisha matokeo yaoya insha katika mwaka huu, ukweli ni kwamba, matokeo yao yalikuwa bado chini ya alama ya wastani ambazo ni 20%.

Kwa kawaida matokeo ya insha hujumuishwa pamoja na matokeo ya mtihani wa lugha. Hivyo, matokeo ya mtihani wa insha yakiwa mabaya, basi yataadhiri matokeo ya mtihani wa lugha hata yawe mazuri kwa kiasi gani. Kwa mfano, wanafunzi hawa wa shule ya msingi ya kihumbuni walipata asilimia 28.70 katika mtihani wa lugha mnamo mwaka wa 2011; mnamo mwaka wa 2012, wanafunzi hawa walipata asilimia 29.50% katika mtihani wa lugha. Tunapotazama matokeo ta mtihani wa lugha mnamo mwaka wa 2013, tunapata kuona kuwa wanafunzi hawa walipata alama 27.09%. Baada ya kuzijumuisha alama hizi za matokeo ya mitihani ya lugha pamoja na yale ya mitihani ya insha, tunapata kuona kuwa, wanafunzi hawa hawakumudu kufikisha asilimia 50% ambayo ndio asilimia ya wastani.

Kwa kuzingatia tambia mwandamano za matokeo haya ya mitihani ya kiswahili katika shule hii, ni bayana kuwa, wanafunzi hawa huishia kutofanya vizuri katika somo la kiswahili mtihani wa kitaifa unapojiri.

***SHULE YA UPILI YA KABETE VET: MATOKEO YA MTIHANI WA MWIGO 2011-2013***



Shule ya msingi ambayo tuliishia kuchanganua matokeo yake ilikuwa shule ya msingi ya Kebete Vet. Shule hii pia iko katika eneo bunge la Westlands. Hivyo wanafunzi wa shule hii ya msingi pia wanaweza kukumbana na athari za lugha ya sheng katika mitihani yao. Kwa mtazamo wa data zetu, ni bayana kuwa wanafunzi hawa vilevile huwa hawafanyi vizuri katika mitihani yao ya somo la kiswahili hasa katika kitengo cha uandishi wa insha.

Mnamo mwaka wa 2011, wanafunzi wa shule hi ya msingi walipata alama asilimia 14.50% katika insha. Hii ikiwa na maana kwamba hawakufanya vizuri katika somo hili.




Mnamo mwaka wa 2012, wanafunzi hawa pia hawakufanya vizuri katika somo la uandishi wa insha. Asilimia waliopata ilikuwa 17.02% ingawaje kuna kuimarika kwa matokeo ya mwaka huu ikilinganishwa na matokeo ya mwaka wa 2011 lakini bado wanafunzi hawa hawakuawahi kufikisha asilimia 20%, alama ambazo ni za wastani. Hivyo kuimarika kwao hakukuzua mabadiliko yoyote yale ya kimsingi.

Mnamo mwaka wa 2013, vile vile wanafunzi wa shule hii hawakufanya vyema katika mtihani huo. Wanafunzi wa shule hii walipata alama 17.88. kuimarika kulikuwa kwa asilimia 0.86% kwa ufupi, ni wazi kuwa wao hawakumudu kufikisha ala za wastani ambazo ni 20%.

Matokeo haya kwa jumla yanatupatia mtazamo mbele kwamba wanafunzi hawa huwa hawafanyi vizuri katika mitihani yao ya kitaifa punde inapojiri. Kama tu tulivosema hapo awali kuwa matokeo ya insha hujumuishwa pamoja na matokeo ya mtihani wa lugha. Hivyo basi, kama matokeo ya mtihani wa insha yatakuwa mabaya basi matokeo hayo yataathiri matokeo ya mitihani wa kiswahili kwa ujumla wake.

Baada ya kuyajumuisha matokeo ya mitihani ya insha na yale ya mitihani ya lugha, data zetu zilitubainishia kuwa wanafunzi hawa wa shule hii ya msingi ya Kabete Vet, hawakumudu kuhitimisha alama ya asilimia 50% ambayo ndiyo alama ya wastani. Ni matokeo kama haya ambayo yanatupatia taswira kamili kwamba wanafunzi hawa hawafanyi vizuri katika mitihani ya Kiswahili ya kitaifa punde inapofika. Sababu za kutofanya vizuri katika somo hili zilikita katika matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi hasa shuleni. Kwa nini tunasema hivi? Tunasema hivi kwa sababu wanafunzi hawa hujumuisha mazungumzo ya kisheng katika uandishi wa insha zao. Matokeo yake huwa kwamba, sarufi husika huwa si sanifu rasmi tena.

**SHULE YA MSINGI YA KANGEMI: MATOKEO YA MTIHANI WA MWIGO 2011 -2013.**



Shule ya tatu ambayo tuliweza kuchanganua matokeo yake ya mitihani wa kiswahili ni shule ya msingi ya Kangemi. Matokeo ya mitihani ya Kiswahili katika shule hii, pia yalifuata mtindo ule ule wa kutofanya vizuri hasa katika somo la kiswahil; uandishi wa insha.

Kulingana na matokeo ya mtihani wa insha katika mwaka wa 2011, wanafunzi husika hawakufikisha alama za wastani ambazo ni asilimia 20% katika mwaka huu, wanafunzi walifaulu kupata asilimia 16.56%, zikiwa ni alama za mtihani wa insha.


Tathmini za matokeo ya insha mnamo mwaka wa 2012 zinaonyesha kuwa, wanafunzi wa shule hii vile vile hawakufaulu kufanya vizuri katika mtihani wa insha. Wanafunzi hawa walimudu kupata asilimia 15.36% uchanganuzi wa matokeo haya unaonyesha kwamba wanafunzi hawa walifanya vibaya katika mtihani wa insha ikilinganishwa na matokeo ya mwaka uliotangulia.

Matokeo ya mtihani wa insha katika mwaka wa 2013 vile vile hayakuwa mazuri. Wanafunzi waliofanya mtihani wa insha. Katika mwaka huu vile vile hawakufaulu kufanya vizuri.

Wanafunzi hao walimudu kupata alama za asilimia 16.30% kwa jumla, matokeo ya mitihani ya insha ya wanafunzi hawa hayakuwa mazuri tangia mwaka wa 2011-2013. Wanafunzi tuliowahoji walidai kuwa uandishi wa insha ni swala ambalo huwatia kiwewe sana. Sababu msingi walioitoa ni kuwa muda ambao wao hupewa wa kuandika insha huwa mfupi sana. Lakini ukweli wa mambo ni kuwa, wanafunzi hawa huwa hawafanyi vizuri katika somo hili kwa sababu za matumizi ya istilahi za Sheng katika uandishi wa tungo zao. Vile vile, wanafunzi hawa huwa hawapendi kuchoka, wao hupenda kuandika kwa lugha ya mkato mradi ujumbe ukamilike, ueleweke na umfikie anayetarajiwa kifikiwa. Mambo haya tuliyobaini kwa misingi ya ya uchanganuzi wa data zetu.

***SHULE YA MSINGI YA NEW KIHUMBUNI: MATOKEO YA MTIHANI WA MWIGO***

***2011 -2013.***



Shule ya msingi ya mwisho ambayo tulichanganua matokeo ya mitihani yake yake ya somo la Kiswahili ni shule ya msingi ya New Kihumbuini. Data zetu zilitubainishia vile vile kwamba

wanafunzi wa shule hii ya msingi huwa hawafanyi vizuri katika somo la Kiswahili. Kitengo cha uandikaji wa insha.

Tathimini ya data zetu ilituonyesha kwamba wanafunzi wa shule hii walifanya vibaya katika uandishi wa insha mnamo mwaka wa 2011. Katika mwaka huu, wanafunzi husika walipata alama za asilimia 16.70% zikiwa ni alama za somo la uandikaji wa insha. Hii ina maana kwamba wanafunzi waliofanya mtihani huo hawakufanya vizuri, walianguka.

Mnamo mwaka wa 2012, mambo yalikuwa ni yale yale. Wanafunzi husika hawakufaulu kupita mtihani wao wa insha. Wao pia walipata alama ambazo hazikufikia kiwango cha wastani ambacho ni asilimia 20%. Alama walizipata katika mtihani huo ni asilimia 15.33 alama hizi zilikuwa na upungufu wa takribani asilimia 5% ili kufikia kiwango cha wastani cha asilimia ishirini. Hivyo wao pia walifanya vibaya katika mtihani huo.

Matokeo ya mtihani wa Kiswahili kwa wanafunzi wa mwaka wa 2013 pia hayakuwa mazuri. Wanafunzi hao vile vile walianguka. Alama ambazo wao walizipata zilikuwa asilimia 16.16%. hivyo wao pia walianguka. Hawakumudu kufanya vizuri.

## **HITIMISHO**

Kwa ujumla tunapata kuona kwamba wanafunzi wa shule hizi zote nne huwa hawafanyi vizuri katika somo la Kiswahili. Hali hii inatokana na ukweli kwamba wanafunzi hawa huwa na upungufu wa kutofanya vizuri katika mtihani wa somo la insha. Alama ambazo wao huzipata katika somo hili huwa sio za kuridhisha. Wao hupata alama zilizo chini ya wastani yaani chini ya

asilimia 20%. Hivyo alama hizi huishia kuziathiri alama za mtihani wa lugha. Kwa kawaida alama za mtihaniwa lugha na zile za mtihani wa insha hujumuishwa pamoja ili kupata alama jumla za somo la Kiswahili. Ni kutokana na hali hii ambapo somo la Kiswahili huishia kutofanya vizuri kwa jumla.

Sababu msingi ambazo huwafanya wanafunzi hawa kutofanya vizuri katika mtihani wa insha ni zile zile sababu ambazo tulizichanganua katika kitengo cha vielelezo vya insha. Wanafunzi hawa huwa wameathirika sana kwa misamiati ya Sheng katika uandishi wao wa insha. Hii ina maana kwamba, wanafunzi hawa hujumuisha istilahi za Sheng katika insha zao. Hali hii huchangia kuwepo kwa sarufi isiyo sanifu katika insha hizo zao. Matokeo yake ni kwamba, watahini wa insha kama hizo huwanyima alama nzuri. Watahini hawa huwanyima alama sio kwa misingi ya tathmini zao binafsi ila kwa misingi ya tathmini zilizopendekezwa na kuidhinishwa na wizara au baraza husika la utungaji na usahihishaji wa mitihani ya insha.

Hivyo ni bayana kuwa wanafunzi wa shule hizi huenda wakaendelea kufanya vibaya katika mitihani ya somo la Kiswahili mradi tu, matumizi ya lugha ya Sheng mashuleni, nyumbani, kwenye kumbi za umma na kwenye vyombo vya habari hayatapigwa marufuku. Kwa mtazamo wetu, matokeo ya mitihani ya Kiswahili bado yataendelea kuwa mabaya hata zaidi, hasa katika miaka ijayo.

Katika sura inayofuatia, tunaenda kuchanganua mahitimisho ya utafiti wetu. Mahitimisho hayo yanaenda kukita katika matokeo ya sura ya pili, sura ya tatu na sura ya nne.

## SURA YA TANO

### 5.1 MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Katika sura hii ya tano tumeangazia matokeo ya utafiti wetu pamoja na maswala ibuka. Mambo yote haya yamelenga fika mathumuni ya utafiti wetu. Vile vile matokeo ya utafiti wetu yalilandana na haipotesia zetu za utafiti. Lengo kuu la utafiti wetu lilikuwa kutathmini kama kweli lugha ya Sheng ina athari zozote hasi katika elimu ya msingi kwa wanafunzi wetu. Ari ya utafiti wetu iliongozwa na sababu kwamba yamekuwepo madai mbalimbali kwamba wanafunzi wa shule za msingi wanafanya vibaya katika mitihani yao ya kitaifa ya somo la Kiswahili kutokana na sababu za Sheng. Hivyo tulioamua kulifanyia dai hili utafiti ili kubaini ukweli wake.

Katika sura ya kwanza tuliweka bayana misingi ambayo ingetuongoza katika kufikia makusudio na malengo ya utafiti wetu. Misingi hii ilikuwa pamoja na : tatito la utafiti, mathumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada husika, upeo na mipaka ya utafiti, msingi wa nadharia, yalioandikwa kuhusiana na mada husika, njia za utafiti na umuhimu wa utafiti huu kwa watafiti wajao au washika dau wa nyanja ya elimu

Hivyo katika sura hii ya kwanza, tuliweza kuanagazia wataalamu na wanataaluma kadha wa kadha ambao wamewahi kulizungumzia swala hili la Sheng. Miongoni mwa wataalamu hawa tuliwazungumzia ni pamoja na Ayub Mukwana, Iribemwamgi, Mbaabu, Mazrui, Mitchell na Anthony, Philip Mahu, Abdulaziz, Osinde na Momanyi. Wote hawa tumewataja pamoja na miaka ya kazi zao. Madai yao ndiyo hasa yalitupatia mwongozo mwema wa kuufanya utafiti wetu. Sababu ni kuwa, wote hawa wameizungumzia Sheng katika mitazamo mbalimbali isipokuwa athari za Sheng katika Nyanja ya elimu. Ni kutokana na sababu hizi ambapo sisi kama

watafiti tuliamua kuutafiti ukwele ambao ungetuongoza katika kuzijua na kuzielewa fika athari za lugha hii katika nyanja mbalimbali za elimu. Hivyo, tulikita utafiti wetu katika shule za msingi hasa za umma, ili kubaini kama kweli lugha ya Sheng imechangia kuwepo kwa matokeo mabaya ya somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi.

Utafiti wetu ulitubainishia kwamba, ingawaje ziko sababu kadha wa kadha ambazo huwafanya wanafunzi wa shule za msingi kutofanya vizuri katika mitihani yao ya kitaifa ya shule za msingi, lugha ya Sheng ni mojawapo wa sababu hizo. Lugha ya Sheng ndio lugha ambayo inatawala mazingira ya mwanafunzi wa shule za msingi. Ni kutokana na sababu hii ambapo wanafunzi hawa wa shule za msingi huibeba lugha hii kutoka katika mazingira yao ya malezi awali, na kuiingiza katika mazingira ya shule. Mazingira ya shuleni kwa kawaida yana utofauti na mazingira yasiyo ya shule kikaida. Hivyo matokeo ya uoanishaji wa mazingira haya mawili katika kutimiza wajibu wa kumwelimisha mwanafunzi ndio huwa chanzo cha mwanafunzi wa shule ya msingi kutofanya vyema katika mtihani wake wa Kiswahili katika kiwango cha kitaifa. Hivyo ndivyo utafiti wetu ulivyotubainishia.

Katika sura ya pili tuliangazia mbinu mbalimbali ambazo wanajamii wa lugha ya Sheng huzitumia katika kuunda misamiati yao. Mbinu tulizozibaini ni mbinu bia ambazo lugha takriban zote za ulimwengu huzitumia katika uundajiwa leksimu. Mbinu hizi za uundaji wa maneno ni pamoja na ukopaji na utohozi, Mbinu ya ukatizaji, mbinu ya uambishaji, mbinu ya ubadilishaji silabi, onamatopia, upolisemia, ubunifu wa leksimu, akronimu, tafsiri mkopo, uhulutishaji, uambatishaji, unyambuizi kapa na ujenzi ghairi.

Miongoni mwa mbini hizi bia za uundaji wa maneno, zipo mbinu ambazo hazitumiwi na sheng. Hata hivyo, nyingi ya mbinu hizi zinamilikiwa na kutumiwa na lugha hii ya Sheng. Hivyo lugha ya Sheng ina uwezo wa kujitungia maneno kama ilivyo tu na lugha nyinginezo. Hapa, tuna maana kwamba lugha ya Sheng ni lugha kamili na si kijilugha kama inavyodaiwa na wanataaluma kadha kama vile Iribemwangi. Sababu ya kusema hivi ni kwamba kwa misingi ya misamiati hii, lugha ya Sheng huwa na uwezo wa kufanikisha mawasiliano miongoni mwa wanajamii wake husika.

Utafiti wetu pia ulitubainishia kwamba katika eneo hili la Kangemi hakuna mwanafunzi hata mmoja wa shule ya msingi ambaye hajui neno angalau moja la Sheng, na maana kamili ya neno hilo. Twasema hivi tukiwa na maana kwamba yapo maneno ya Sheng ambayo hukopwa kutoka lugha ya Kiswahili. Maneno haya kisha hupewa maana badala yaliyotofauti na maana kamili ya maneno hayo katika lugha ya Kiswahili. Mifano ya maneno kama haya ni kama vile neno “Chuo.” katika Kiswahili, neno hili huwa na maana mbalimbali. Mojawapo ya maana kamili ya neno hili ni pamoja na: kiwango cha elimu baada ya shule ya upili. Lakini katika Sheng neno “chuo” lina maana msingi ya kiwango chochote kile cha elimu. Neno hili wanalijua wanafunzi wengi wa shule za msingi ila kwa misingi ya maana ya Sheng. Vile vile, neno hili ni neno maarufu sana miongoni mwa wanafunzi hawa wa shule za msingi.

Katika sura ya tatu, tumeshughulikia nyenzo mbalimbali ambazo wanafunzi wa shule za msingi hujifunza Sheng kutokana nazo. Nyenzo ambazo tulizibaini kutokana na utafiti wetu ni pamoja na vyombo vya habari kama vile televisheni na redio, wazazi, waalimu, ndugu na wanafunzi wenza. Ni kutokana na nyenzo hizo ambapo wanafunzi wengi wa shule za msingi hupata kujifunza



Sheng. Kulingana na nyenzo hizi ni bayana kwamba nyingi yazo inapatikana katika mazingira ya kwanza ya ulezi wa mtoto na wala sio shuleni. Hivyo mwanafunzi anapohitimu umri wa kujiunga na shule, tayari huwa na msingi wa kujifunza na kuongea Sheng. Ingawaje katika kiwango hiki, uwezo wa mwanafunzi wa kuongea Sheng huwa finyu mno, lakini uwezo huo huanza kupanuka jinsi anavyozidi kuvuka daraja moja la elimu hadi lingine na kadri miaka yake inavyozidi kuongezeka.

Kule shuleni, mwanafunzi huyu hupatana na nyenzo nyingine za ujifunzaji wa Sheng. Nyenzo hizi huwa ni pamoja na walimu chipukizi na wanafunzi hasa wale wa madarasa ya juu. Kati ya nyenzo hizi mbili- yaani walimu na wanafunzi wenzi. Wanafunzi limbukeni huweza hasa kujifunza Sheng kutokana na wanafunzi wenza. Ujifunzaji huu wa Sheng hutokea kama sehemu ya elimu isiyo pangilizi. Hivyo marafiki na viranja wa mwanafunzi huyu huweza kumsheheni kwa leksimu mbalimbali za Sheng. Hivyo, mwanafunzi huyu anapohitimu umri wa kujiunga na dara la sita, saba na nane, huwa amekolea kwa misamiati ya lugha hii. Ni katika darasa hili la nane ambapo mwanafunzi huyu hutarajiwa kuufanya mtihani wake wa kitaifa wa darasa la nane. Miongoni mwa mitihani hiyo, huwemo mtihani wa somo la Kiswahili ambalo huja kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza hujumuisha maswali ya lugha na ile ya pili hujumuisha uandishi wa insha.

Ni katika awamu ya uandishi wa insha ambapo mwanafunzi huyu huishia kutofanya vizuri. Sababu ya kutofanya vizuri kwa mwanafunzi huyu hutokana na ujumuishaji wa leksimu za Sheng na zile za Kiswahili sanifu katika insha yake. Ni hali kama hii ambayo huonekana na watahini kama uchafuzi wa lugha ya Kiswahili sanifu. Hivyo mwanafunzi husika huishia kupata

alama zisizoridhisha katika somo zima la Kiswahili. Matokeo yake huwa kwamba mwanafunzi husika huishia kulianguka somo la Kiswahili. Hivi ndivyo utafiti wetu ulivyotubainisha.

Katika sura ya nne, tumechanganua data za matokeo ya mitihani ya Kiswahili ya kitaifa. Katika uchanganuzi huo wetu, tumechanganua kwa kudhihirisha wazi matokeo ya somo hili kwa kukita katika shule za msingi zifuatazo: shule ya msingi ya Kabete Vet, shule ya msingi ya Kangemi, shule ya msingi ya Kihumbuini na shule ya msingi ya New Kihumbuini. Katika uchanganuzi huo wetu tulipata kubaini kuwa wanafunzi wa shule hizi za msingi huwa hawafanyi vyema katika mitihani yao ya kitaifa ya Kiswahili. Ingawaje tatizo hili hujidhihirisha katika kitengo cha mtihani wa lugha, athari nyingi zilikita katika mtihani wa uandikaji wa insha. Hivyo alama za insha - ambazo huwa mbaya - huziathiri zile za lugha. Ni jambo hili ambalo huwafanya wanafunzi hawa kutofanya vizuri katika mtihani wa somo la Kiswahili kwa jumla.

Shule hizi nne tulizozifanyia au tulizozitumia katika kielelezo cha utafiti wetu zinapatikana katika maeneo duni ya maakazi hapa kangemi. Wakazi wengi wa maeneo haya ni watu wenye mapato madogo ya kiuchumi. Yaani ni watu maskini. Ikumbukwe kuwa, Haya ndio maeneo yanayosadikika kuwa chimbuko na asili ya lugha ya Sheng katika mitaa duni ya mashariki mwa jiji la Nairobi. Hivyo hali hii vile vile inajidhihirisha katika eneo bunge hili la Kangemi. Yaani, Sheng ni lugha inayozungumzwa na watu wa tabaka la chini kiuchumi.

Majina ya maneno ambamo shule hizi zinapatikana ni pamoja na Gishagi, St. Joseph, Fly over, Sodom, Gitoka, Botom line, Uthiru, Kibagare na Michigan. Haya ndio mazingira yanayowazaa na kuwalea wanafunzi hawa wanaojiunga na shule hizi za msingi. Mazingira haya ni yale yenye

sifa za wanajamii wanaozungumza Sheng. Hivyo wanafunzi hawa ambao huwa zao la mazingira haya wanapohitimisha umri wa kujiunga na shule, wao huwa na huo uwezo wa angalabu kuizungumza Sheng, hata kama si kwa mfululizo vile. Athari za mazoea haya hujidhihirisha baadaye pale mwanafunzi huyu huhitimisha umri wa kujiunga na darasa la nane. Yaani mwanafunzi huyu ambaye ni zao la jamii hii inayozungumza Sheng huishia kutofanya vizuri katika mtihani wake wa Kiswahili. Hali hii husababishwa na mazoea ya matumizi ya Sheng nyumbani na shuleni. Hivi ndivyo utafiti wetu ulivyotubainisha.

## **5.2 Mambo Ibuka**

Ingawaje utafiti wetu ulilenga kubaini kama Sheng ndio huwa chanzo cha matokeo mabaya ya somo la Kiswahili katika shule za msingi, utafiti wetu pia ulituwezesha kubaini jambo jingine msingi ambalo halikuwa sehemu ya utafiti wetu. Jambo hili ni kuwa wanafunzi wengi wa shule za msingi huwa hawaichukulii lugha ya Kiswahili na vile vile somo la Kiswahili kwa uzito ambao lugha hii inahitaji. Hali hii ya kukipuuza na kukidunisha Kiswahili hujidhihirisha miongoni mwa walimu, wazazi na wanafunzi. Walimu hupendelea sana wanafunzi kuzungumza na kuwasiliana kwa lugha ya kingereza kuliko Kiswahili. Hali hii hujidhihirisha vyema kwenye ratiba kuu ya masomo katika shule hizi. Hapa masomo yote isipokua somo la Kiswahili hufundishwa kwa lugha ya kiingereza. Vile vile, lugha ya mawasiliano katika shule hizi huwa lugha ya kingereza kwa angalabu siku nne au tano za wiki. Mwanafunzi ambaye hupatikana na hatia ya kuvunja amri hii huadhibiwa. Hali hii wakati mwingine huwafanya wanafunzi hawa kuuliza au kujibu maswali katika lugha ya kingereza hata kama kipindi husika ni cha lugha ya Kiswahili.

Kule manyumbani , wazazi hufurahia sana wanapowasikia watoto wao wakiwasiliana kwa lugha ya kiingereza. Kwao, hali hii huwa ni dhihirisho tosha kuwa watoto wao kweli wanasoma na wameanza kustaarabika . Watoto hawa hata wanapozungumza kiswahili sanifu kule nyumbani, hali hii huwa haiwashawishi wazazi kuelewa kuwa, kweli watoto wao wanasoma au wanasoma masomo shuleni.

Hivyo basi wanafunzi hawa hata wanapozungumza Kiswahili kilichochanganyikana na misamiati ya Sheng kwao hili huwa si kosa kubwa au linaloweza kusababisha mwanafunzi kutofanya vizuri katika mtihani wake wa somo la Kiswahili. Ni mitazamo kama hii ambayo kwa hakika imechangia ukuaji na uwenezaji wa lugha ya Sheng miongoni mwa watoto au wanafunzi hawa wa shule za msingi.

Wanafunzi pia wana mchango wao katika uchukulizi huu. Wao huwa hawatilii maanani uzungumzaji wa Kiswahili sanifu. Kwao Kiswahili sanifu ni milki ya wakazi wa pwani ya Kenya na Tanzania. Vile vile wanafunzi hawa huongozwa na imani potovu kwamba somo la kiswahili ni somo rahisi; si somo ngumu kama vile hisabati, kingereza au sayansi. Hivyo nguvu zao nyingi wao huzielekezea masomo haya kwa gharama za somo la Kiswahili. Haya tuliyabaini kutokana na uchanganuzi wa data zetu.

### **5.3Mapendekezo Ya Utafiti**

Sheng na athara zake ni swala ibuka katika Jamii yetu. Sheng ni lugha ambayo si sehemu ya lugha asili zinazopatikana nchini Kenya. Lugha hii imezuka tu hivi karibuni. Ingawaje lugha hii ni lugha shuka, inafaa ieleweke vyema kwamba tayari lugha hii ina wazungumzaji wengi hata

kuliko lugha fulani za kiasili nchini Kenya. Hivyo lugha hii inao uwezo wa kusababisha athari nyingi sana katika asasi mbali mbali za Jamii yetu.

Utafiti wetu ulikita katika asasi ya elimu , kiwango cha shule za msingi. Hivyo hatukugusia athari ya lugha hii katika asasi ya elimu , kitengo cha shule za upili, vyuo vya anuwai na vyuo vikuu. Hivyo tunapendekeza kwamba watafiti wajao waweze kutafitia athari za lugha ya Sheng katika viwango hivi vya elimu. Huwenda ikawa kwamba athari zake ni finyu au ni pana sana katika vitengo hivi vya nyanja ya elimu.

## MAREJELEO

- Abdulaziz, M. na K. Osinde, (1997), "*Sheng and English in Nairobi: Development of Mixed Codes among the Urban Youth in Kenya.*" International Journal of the Sociology of Language 125:43-63
- Bosire, M. (2008), *Sheng. The Phonological and Social Profile of an Urban Vernacular*. Tansifu ya Uzanifu ambayo haijchapishwa: University of Albany. State University of New York.
- Githinji, P. (2008), *Language Attitudes: Nairobi People and Sheng*. Tansifu ya Uzamili ambayo bado haijchapishwa, Michigan State University.
- Hartman R. K. na F. C. Stork, (1972), *Dictionary of Language and Linguistics*. London: Applied Science Publishers Ltd.
- Hudson, R. A. (1996), *Sociolinguistics*, (2<sup>nd</sup> Edition) Combridge, C. U. P.
- Iribemwangi, P. I. & A. Mukhwana, (2011), *Isimujamii*. Nairobi. Focus Publishers Ltd.
- Karanja, M. N. (1993), *Miaka 50 Katika Jela*. Nairobi: Heineman Kenya
- Katamba, F. (1993), *Morphology*. Cambridge University Press.
- Katie, W. (2001), *A Dictionary of Stylistics*. Longman: Halow.
- Kembo-Sure, (1992), "*The Coming of Sheng,*" English Today 26 – 28
- King'ei, G. K. (2001), Language and Identity. The Challenge of Sheng in Kenya. Paper presented at the Association of Third World Studies Conference, September 17-19, 2001, Njoro, Egerton University, Kenya.
- Makokha, W. O. (2010), Uchanganuzi wa Kiisimu wa Baadhi ya Matini za Kiswahili. Mtazamo wa Pragmantiki KLeksika. Nairobi, Tansifu ya Uzamili ambayo bado haijchapishwa.

- Mathews, P. H. (1997), *A Concise Dictionary of Linguistics*. New York, Oxford University Press.
- Mazrui, A. M. (1995), “*Sheng and Code Switching: The Case of Sheng in Kenya.*” *Africanistich Arbeitspapier* 41: 168 – 179
- Mbaabu, I. na K. Nzuga, (2003), *Sheng-English Dictionary: Deciphering East Africa’s Underworld Language*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mgesa, M. (2002), *And Sheng Lives on Profile*. East African Standard 16 – 22, Feb 2001.
- Mgullu, R. S. (1999), *Mtalaa wa Isimu, Fonestiki, Fonologia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Moga, J. na D. Fee, (1993), *Sheng Dictionary*. Nairobi: Ginshen publishers.
- Momanyi, C. (2009), “*The Effect of Sheng in the Teaching of Kiswahili in Kenyan Schools.*” *The Journal of Pan African Studies*, 12: 127 -138.
- Mukhwana, A. (2008), *Language Attitude in Urban Kenya: A Case Study of Nairobi, Mombasa and Kisumu*, Tansifu ya uzanifu ambayo bado haijachapishwa.
- Obuchi, S. M. na A. Mukhwana (2010), *Muundo wa Kiswahili; Ngazi na Vipengele*. Nairobi: Frame Publishers.
- Ogechi, N. O. (2002), *Codeswitching in Kenya Evidence from Ekegusii, Kiswahili, English and Sheng*. Tansifu ya Uzanifu ambayo haijachapishwa. Hamburg: University of Hamburg.
- Ogechi, N. O. (2005): “*Lexicolization in Sheng.*” *Nordic Journal of African Studies* 14(3), 334 – 355.
- Osinde, K. (1986), *Sheng; An Investigation into the Social and Structural Aspects of An Evolving Language*. Tansifu ya B. A. ambayo bado haijachapishwa. Nairobi: Chhuo Kikuu cha Nairobi.

- Richards et al, (1985), *Longman Dictionary of Applied Linguistics*. U. K., Longman Group.
- Samper, H. (2002), *Taking Sheng: The Role of Hybrid Language in the Constitution of Identity in Youth Culture in Nairobi, Kenya*. Tansifu ya Uzanifu ambayo bado haijachapishwa, University of Pennsylvania.
- Saussure, F. (1916), *Course in General Linguistics*. London: Duckworth.
- Shitemi, N. L. (2002). “*Pidginization Sheng, The Melting-pot of the Kenyan Language and an Anti-Babel Development.*” *Kiswahili* 64: 1 – 15.
- Spyropoulos, M. (1987). “*Sheng: Some Preliminary Investigation into a Recently Emerged Nairobi Street Language.*” *Journal of the Anthropological Society at Oxford*, 18 (18) 125 – 136.
- Trudgil, P. (1974), *Sociolinguistics: An Introduction to Language and Society*. England: Penguin Books.
- Ullmann, S. (1957), *The Principle of Semantics*: Great Britain: Britain: Blackwell and Mott.
- Ullmann, S. (1962), *Semantics. An Introduction to Science of Meaning*. Great Britain: Blackwell and Mott.
- Wilson, D. na D. Sperber, (2002), *Truthfulness and Relevance*. *Mind*. 111.



**KIAMBATANISHO I:**  
**KIAMBATISHO HOJAJI**

Mimi ni mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika chuo kikuu cha Nairobi ambapo nasomea lugha ya Kiswahili. Zipo tetesi kuwa Sheng inaathiri matokeo ya mtihani wa Kiswahili katika shule za msingi mtaa wa Kangemi. Nimekuja kwako ili nikuombe unijazie hojaji hii ili nijue hali halisi ya lugha ya Sheng haswa mtaani kangemi.

Majibu yako yatasaidia kuiboresha kazi yangu na kuipa mwelekeo na mkabala. Majibu yako yatakuwa ni ya siri sana na wala hayatatolewa kwa yeyote.

**SEHEMU: A. MAELEZO KUHUSU MTAFIGITIWA**

1. Jinsia
2. Kiwango cha elimu
3. Umri
4. Shule / chuo
5. Umilisi wa lugha. Wewe ni msemaji was lugha zipi? Kiswahili, Sheng, Kiingereza au lugha za kienyeji

**SEHEMU B:**

Matumizi ya lugha katika jamii ni jambo ambalo halina budi ila kutimiziwa. Lugha mbalimbali hutumika katika nyanja tofauti tofauti. Ikiwemo elimu. Lugha zinazotumika ni Kiingereza na Kiswahili. Kama mhusika katika jamii utakubaliana vipi na maswala haya?

**(ELEZA KWA USEMI HALISI)**

1. Kwa maoni yako, Sheng ni nini?
2. Sheng hutumiwa na akina nani?
3. Kwa nini Sheng hutumiwa?
4. Sheng hutumiwa sana na jinsia gani? (ya kike au kiume)
5. Kwa sababu gani?
6. Je, matumizi ya Sheng hutofautiana kulingana na jinsia?
7. Sheng ina hadhi gani katika jamii mtaa wa kangemi? (ya juu au ya chini?)
8. Kwa nini baadhi ya Sheng iwe jinsi ilivyoeleza hapa juu?
9. Taja majukumu ya Sheng kama inavyotumika katika mtaa wa kangemi.
10. Je, Sheng hutofautiana kimatumizi katika maeneo mbalimba kama vile shuleni, nyumbani, kanisani, sokoni, msikitini na kadhalika mtaani kangemi?
11. Kama hutofautiana, toa mifano jinsi ambavyo Sheng hutofautiana.
12. Je: Sheng imeathiri matokeo ya mtihani wa Kiswahili katika shule za msingi mtaani Kangemi.
13. Kama imeathiri kivipi? Toa Maelezo.
14. Kulingana na maoni yako panga lugha kihathi kuanzia juu hadi chini.
  - a) Lugha ya Kiswahili
  - b) Lugha ya kikabila
  - c) Lugha ya kingereza
  - d) Lugha ya Sheng
  - e) Lugha nyingine yoyote unoyoifahamu

15. Je, Sheng hutumiwa na akina nani na kwa nini shuleni?

16. Je, Sheng ni lugha ambayo inakua au inadidimia?

17. Lugha gani huhusishwa na

- a) Wasomi
- b) Vijana
- c) Watu wasiosoma
- d) Wenye hadhi ya chini au juu
- e) Mawasiliano ya kawaida
- f) Wazee
- g) Watu wa mjini
- h) Kupitwa na wakati
- i) Ujuaji
- j) Biashara
- k) Siasa
- l) Dawa za kulevya

18. Kwa nini lugha hizi huhusishwa na watu uliotaja hapo juu?

19. Kulingana na maoni yako, kipo kisababishi kingine cha matokeo mabaya ya mtihani wa

Kiswahili katika shule za msingi mtaani kangemi? Eleza.